# *Mtu Aliyeitwa Na Mungu*

. . . Neville. Ni masikitiko tu kuwaweka mmesimama, kando ya kuta. Nami nilipitia hapa kwenye miadi nyingine, yapata saa moja na nusu iliyopita, nao watu walikuwa wakigeuka kutoka mlangoni, wakienda zao. Nilikutana na Billy kule nje, naye akasema mahali hapa palikuwa tayari kwa ajili ya ibada kuanza, tangu alasiri ya leo. Kwa hiyo mimi . . . Ndio kwanza tuwe na mkutano huu mdogo hapa. Hata hatukuuweka kwenye magazeti ya huku. Kwa hiyo, tuna muda kidogo tu wa ushirika.

2 Na sasa sikuzote ni shughuli nyingi, kama vile watu wa nje ya mji wangejua, kwamba, humu nyumbani sikuzote ni kuruka-ruka, kukimbia mahali mahali, na msukumano. Kwa hiyo, kidogo ninakuzoea. Ninafika mahali ambapo siliruhusu linisumbue, kadiri niwezavyo. Na unajua, huna budi kutumia muda kidogo tu, na unapaswa kuwa zaidi, pamoja na Bwana. Usipofanya hivyo, basi huji mkutanoni ukiwa na upya wa Roho Mtakatifu. Ndipo unapoingia, kama vile imekuwa leo hii, ambapo imekuwa tu ni kivutio kimoja kikubwa, kikubwa mno, vema, kidogo ni vigumu kwangu kuingia, kuzuia isiwe tu ni kubanwa kidogo na kusukumana, mnaona, na kujifadhaisha. Nikifanya hivyo, basi siwezi kumpata Roho Mtakatifu popote ndani yake.

3 Kwa hivyo, ninasikitika, hata hivyo, kwa ajili ya watu wanaosimama ka—katika marefu ya kanisa na upande wa nje. Nao wanakuja, wanachungulia ndani, wanaingia kwenye gari lao na kurudi. Nilitaka kuchukua shule ya upili hapa chini, kufanya mkutano wa siku chache tu usiku, lakini hiyo shule inaendelea kwa wakati huu, na kidogo ni vigumu kwangu kuipata mnamo wakati huo. Lakini nataka kusema kwamba hakika namthamini kila mmoja wenu, mlio ndani na nje, na kwa ushirikiano wenu mzuri, na kwa yote mliyofanya.

4 Na asubuhi ya leo, katika shule ya Jumapili, niliwashukuru watu kwa ajili ya sadaka niliyopewa jana usiku, ambayo ilikuwa ni sadaka isiyoombwa. Kwa kweli, nilimwambia mchungaji hapa, mchungaji wetu mpendwa, Ndugu Neville, na hao wengine, afadhali wasingefanya hivyo. Lakini walifanya hivyo, hata hivyo, kwa hiyo nilitaka tu kutoa taarifa yake. Sasa, hapa ni mahali padogo, napo hapatakaa zaidi ya watu yapata mia tatu, sidhani. Nayo hiyo sadaka ilikuwa dola mia tatu ishirini na nne, ambayo ina maana kwamba walikuwa na wastani wa dola moja kwa kila mtu. Hiyo ndiyo sadaka bora zaidi niliyowahi kupewa maishani mwangu, kwa hiyo idadi ya watu. Kwa kawaida, itakuwa na wastani wa senti ishirini na nne kwa mtu, ishirini na tano. Senti ishirini na saba ni sadaka kubwa, kwa mtu. Lakini

hii ilikuwa wastani wa dola moja kwa kila mmoja. Na hakika ninathamini hilo.

5 Na labda sikupata, asubuhi ya leo, kuwaelezea baadhi yenu. Tulipata jeli, sanduku la jeli limewekwa kwenye vipandio, na zawadi ndogo zimetumwa kwetu. Mimi na mke wangu tungependa kutoa shukrani zetu kwenu ninyi watu. Nami nina hakika ya kwamba kadri tujuavyo sisi, yote itakuwa kwa ajili ya Ufalme wa Mungu.

6 Basi inanifanya nijisikie kama laiti ningalikuwa na mahali pazuri ambapo tungeweza kuendelea kwa muda mrefu na kuwahudumia watu. Lakini hata usiku wa leo, baada ya ibada, ninapaswa kuondoka. Ambapo, sitaweza kuondoka usiku wa leo, lakini asubuhi na mapema, niondoke.

7 Nitarudi Jumamosi ijayo usiku. Niondoke Jumapili asubuhi, tena, kuelekea Colorado. Na ni mmoja tu baada ya mwingine, nikienda.

8 Halafu basi mkutano wangu unaofuata wa nchi za ng'ambo unakuja Januari, ambao uko Australia na New Zealand, na kupitia huko. Sasa, nawatakeni mniombee. Hakika natamani maombi yenu.

9 Na kisha nataka. . .sote kumshukuru Mwenyezi Mungu, Yule aliyetufanyia mambo makuu katika mkutano huu mdogo. Ninaamini, kwa huu muda wa wakati, kumekuwa na mengi zaidi yaliyofanikishwa katika mkutano huu kuliko mkutano wowote niliowahi kufanya maishani mwangu kwenye maskani hii. Bwana alionekana tu kuzifungulia baraka.

10 Nimefikiria, labda, muda wote wa mkutano huu, kwamba kutokana na ono ambalo nimekuwa nalo, kwamba huduma yangu itabadilishwa kuwa huduma bora na kuu zaidi. Sasa, itatokea tu kwa hakika tu kama vile ninyi watu mmesikia huduma hizi zingine tatu zikibashiriwa, au hizi zingine mbili. Hii itakuwa tu kama hizo, ila tu kuu zaidi. Lakini usiku wa kwanza, niliwaita tu watu hapa madhabahuni, nikarudi moja kwa moja kwenye upambanuzi. Usiku wa pili, nimewaingiza chumbani, nikaingilia upambanuzi moja kwa moja. Na siku mbili zilizopita usiku, basi, tumewaleta hapa jukwaani, moja kwa moja tu kwenye upambanuzi.

11 Lakini ili tu kutoa taarifa ya mambo fulani, mhudumu mmoja kipofu alifunguliwa macho jukwaani.

12 Kisha wasichana wawili wadogo, jana usiku, walioketi kwenye kiti cha magurudumu, wakiwa na magonjwa ambayo hakuna mtu anayejua ni nini, hakuna daktari. Miguu yao imevimba sana, na vidole vyao vya miguu vikianguka, vidole vya mikono vikianguka, wala wasingeweza kufanyiwa chochote. Ndipo wakati tu Roho alipokuwa akitia mafuta, nilienda pale, na katika Jina la Bwana Yesu, nikaulaani ugonjwa huo, nao hao wakatoka kwenye kiti cha magurudumu. Ndipo asubuhi ya leo,

wakitembea hapa maskanini, kama mtoto mwingine yeyote, na wakaja hapa na kubatizwa kwa ubatizo wa Kikristo, papa hapa kidimbwini, asubuhi ya leo.

13 Wakati, nilikuwa na dakika chache za kusoma, muda mfupi uliopita, na kulikuwako na marafiki zangu, Ndugu Hoover, mhudumu kutoka kule chini Kentucky, wakapita tu na kumwachia mke wangu habari, kwamba jana usiku katika mstari wa wito, huku kwenye kusanyiko, wanawake ambao hawakuwa na kadi zozote za maombi wala chochote kile, wameketi tu huko wakiomba. Basi kulikuwako na mwanamke mmoja ambaye alikuwa hajala kwa, nasahau ni muda gani, mlo; vivimbe tumboni mwake, lote limejaa. Ndipo Bwana akamwita na kumponya. Basi asubuhi ya leo aliamka na kula kiamshakinywa kizima cha kawaida, naye yuko hapa mahali fulani usiku wa leo.

14 Na wengine, aliokuwa akisimulia, na, loo, wakati haungeruhusu, juu ya mambo ambayo Bwana wetu amefanya. Kwa hiyo, kwetu sisi, hilo hutupa ujasiri wa kujua ya kwamba liko karibu tu, jambo fulani liko karibu kutukia, kubwa.

15 Jana jioni, baada ya ibada, baada ya Ujumbe, sijawahi kumwona Roho Mtakatifu wakati wowote akiwapaka mafuta watu zaidi ya alivyofanya jana usiku. Tunatazamia kwingine, usiku wa leo. Na sasa mniombee.

16 Nami nataka kusoma baadhi ya Neno la Mungu lililobarikiwa. Na kabla hatujasoma Neno, hebu na tuzungumze tu Naye, huku vichwa vyetu vimeinamishwa kwa muda kidogo tu.

17 Mpendwa Baba wa Mbinguni, tunakuja Kwako usiku wa leo, labda tukiwa tumechoka tu kidogo mwilini, lakini, loo, jinsi roho zetu zimeburudika! Ishara za Mungu aliye hai, kwamba Yeye yuko pamoja nasi, na anatubariki, na kutupa kile alichoahidi Yeye, sana, kwa wingi, zaidi ya yote ambayo tungeweza kufanya au kufikiria. Na ikiwa tumepata neema machoni Pako, kwa kumwamini Mwanao, Bwana Yesu, tungeomba usiku wa leo ya kwamba Wewe ungetutembelea tena pamoja na sehemu maradufu ya Roho Wako. Na amwagwe kwa nguvu nyingi na vipimo juu ya kila mtu hapa, kuamini Injili na kupokea Nguvu za Roho Mtakatifu katika maisha yao. Okoa wale wanaoweza kuokolewa usiku wa leo, Bwana, na uwaponye wale walio tayari kuponywa. Tujalie, Bwana.

18 Na tunapowaona watu wakiingia ndani, wakisimama milangoni, mamia wakigeuka kwenda zao kutoka kwenye hili kanisa dogo, inatukumbusha kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo na hata milele. Kwamba, katika siku zile alipotutembelea hapa katika umbo la mwili, umati ulikuwa mkubwa sana, hata wasingeweza kumfikia wakiwa na mtu, na ikabidi wamshushe kupitia kwenye paa la hilo jengo. Nasi

tunaomba, Mungu, ya kwamba usiku wa leo, ya kwamba kila mtu ambaye amelazimika kusukumiza kwa njia hii atazawadiwa kama vile mtu huyo alivyozawadiwa.

19 Libariki Neno Lako tunapolisoma. Na jalia liwe Taa, Nuru ya njia yetu. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

20 [Mtu fulani anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] La. Ati Rosella Griffith? ["Naam."]

21 Nimepashwa habari hivi punde tu kwamba msichana niliyemtaja asubuhi ya leo...mlevi sugu aliyekuwa ameitwa mkutanoni huko Chicago. Ilikuwa kwamba alikuwa ameketi kwenye roshani wakati Roho Mtakatifu aliponena naye na kusema alikuwa mlevi sugu. Nao madaktari watano mashuhuri wa Chicago walikuwa wamemkatia tamaa. Shirika la Kusaidia Walevi Sugu lilikuwa limemkatia tamaa. Naye akaitwa hadharani, kwa BWANA ASEMA HIVI. Akaponywa. Hajatamani pombe tangu wakati huo.

22 Ndipo maskini msichana mwingine kwenye roshani juu yake, ambaye alikuwa ni rafiki yake, ambao waliishi katika Jiji la Calumet. Iwapo mtu yeyote anajua hiyo ni nini, huko ni mipakani ambako ni kubaya kuliko Paris, Ufaransa, kila namna ya uovu ikiendelea. Naye akamwambia kwamba alikuwa mchuuzi wa dawa za kulevya, naye alikuwa mcheza dansi pamoja na Fred Astaire. Ndipo baba yake akachukizwa nalo. Lakini yeye akasimama na kusema, "Baba, huyu mtu amesema kweli kabisa." Sasa ameolewa, maskini huyo msichana, na yuko njiani, huko nje pamoja na mumewe, wakiihubiri Injili.

23 Rosella ni mfanyakazi wa misheni, kutoka katika kila huduma ya jela na kila kitu anachoweza kufikia, akiwaambia walevi sugu kwamba kuna tumaini, na hilo liko katika Kristo.

24 Amekuwa na mzigo mkubwa sana kwa ajili ya baba yake. Si zaidi ya majuzi tu, kwenye mahojiano ya faragha, ya dakika kumi, huyo msichana amekuwa msaidizi dhahiri wa mikutano hii, kwa miaka minne au mitano iliyopita, ambapo aliniambia, katika taarifa ndogo ya dakika kumi, huko nje kwenye trela, kwenye mahojiano, ambapo alisema, "Ndugu Branham, chochote ufanyacho, nimelemewa vibaya sana na mzigo kwa ajili ya baba yangu. Anakupenda, lakini hatamjia Kristo."

25 Nikasema, "Rosella, Mungu anajua jinsi ya kufanya hilo. Anajua jinsi ya kumfanya amjie."

26 Na taarifa imefika sasa kwamba amezikwa chini ya gari lililojaa mawe ya chokaa. Hebu tumwombeeni.

27 Bwana, kwa kinywa cha binti huyo mwaminifu, huku yeye amenaswa kule chini, ambapo angeweza kufia chini yake; Mungu, jalia asife, lakini nafsi yake itaangalia juu na kukumbuka kwamba Wewe ni Mungu anayeweza kujibu

maombi chini ya lundo la mawe ya chokaa, sawasawa na vile ungeweza katika tumbo la nyangumi, au katika tanuru yenye moto, au katika tundu lenye simba. Unabaki yule yule. Mtoe humo, Bwana, Mkristo aliyeoshwa. Tunajua kwamba mambo yote hufanya kazi kwa manufaa ya wale wanaokupenda. Nasi tunaomba ya kwamba hili litakuwa mojawapo ya mambo hayo, tunapolikabidhi Kwako, katika Jina la Yesu. Amina.

28 Katika kusomwa kwa Neno usiku wa leo, katika Kitabu cha Wafalme wa Pili, ningependa kusoma katika mlango wa pili, kwa ajili ya somo dogo tu, kupata muktadha, Mungu akipenda.

> *Ikawa, hapo* B*WANA* *alipoenda kumpandisha Eliya mbinguni kwa upepo wa kisulisuli, Eliya alitoka Gilgali pamoja na Elisha.*
>
> *Eliya akamwambia Elisha, Tafadhali* wewe *kaa hapa; kwa maana* B*WANA* *amenituma niende mpaka Beth-eli. Naye* Eliya *akamwambia, Kama* B*WANA* *aishivyo, na roho yako iishivyo, sitakuacha. Basi wakashuka mpaka Beth-eli.*
>
> *Basi wana wa manabii*. . .*waliokuwa* huko *Beth-eli wakatoka kuonana na Elisha, wakamwambia, Je, unajua ya kuwa* B*WANA* *atamwondoa bwana wako leo asiwe mkuu wako? Akasema, Naam, najua; nyinyi*. . . *nyamazeni.*
>
> *Eliya akamwambia, Elisha, Tafadhali, kaa hapa; kwa maana* B*WANA* *amenituma niende mpaka Yeriko. Akasema, Kama* B*WANA* *aishivyo, na roho yako iishivyo, sitakuacha. Nao* wakaenda *Yeriko.*
>
> *Basi wana wa* nabii. . .*waliokuwa* huko *Yeriko wakamkaribia Elisha, wakamwambia, Je, unajua ya kuwa* B*WANA* *atamwondoa bwana wako leo, asiwe mkubwa wako? Akajibu, Naam, najua; nyinyi*. . . *nyamazeni.*
>
> *Eliya akamwambia, Tafadhali, kaa* hapa, *kwa kuwa* B*WANA* *amenituma niende mpaka Yordani. Akasema, Kama* B*WANA* *aishivyo,*. . .*roho yako iishivyo,* mimi *sitakuacha. Wakaendelea mbele wote wawili.*

29 Bwana na aongeze baraka Zake kwenye Neno Lake. Somo langu la usiku wa leo ni: *Mtu Aliyeitwa Na Mungu*. Nami nitajaribu kuufupisha tu niwezavyo, kwa sababu tuna mstari mkubwa wa maombi unaokuja katika dakika chache tu, lakini, ili tu kuwapeni mtazamo mdogo kwenye nyakati tunazoishi.

30 Tunasikia kilio hiki kwenye redio, na mahali mbalimbali, nacho kikitoka kwenye mioyo miaminifu, "Bwana, tupe uamsho katika wakati wetu." Na kutoka kwenye barua zinazotoka kwa Wakristo ulimwenguni kote, tunasikia kilio hicho, nacho kinafanya jambo fulani moyoni mwako. Inavuvia. Inainua.

Inahuisha, kwa nafsi, kuwasikia watu wa Bwana wakiombea uamsho.

31 Naye Mungu ametoa ahadi, "Ikiwa watu wanaoitwa kwa Jina Langu watakusanyika pamoja na kuomba, basi nitasikia kutoka Mbinguni."

32 Na kwa hiyo sisi, usiku wa leo, tunataka kulitafakari jambo hilo. Basi kumbukeni, ya kwamba, katikati ya kilio hiki chote, Mungu hawezi kutuma uamsho mpaka awe na watu walio tayari kuupokea. Hatuwezi kuwa na uamsho mpaka tupate watu, watu walioitwa na Mungu, watu waliofunzwa na Mungu, ambao hawajafunzwa katika shule za theolojia na za elimu, bali ni watu shupavu wa imani, ambao Mungu amewalea katika shule ya mafunzo Yake magumu. Watu ambao hawaogopi kukabiliana na moto! Watu ambao wamekuja Mbele za Mungu; na wanajua nguvu Zake, na wanajua uweza Wake usio na kikomo, na wanajua nguvu Zake za uponyaji! Watu ambao wamefunzwa kumjua Mungu aliye hai! Ni sawa kuwafundisha kwa Neno, lakini, "Andiko huua; Roho huleta Uzima."

33 Na kabla hatujaweza kuwa na uamsho huu, Mungu hana budi kuwaita watu watoke na kuwafunza, watu waliofunzwa na Mungu, kuubeba Ujumbe huu. Nao hawajali upinzani ni nini. Wako tayari kwenda kwenye tanuru ya moto kwa kushindwa, au kwenye tundu la simba, au popote pale. Wako tayari kwenda, kwa sababu wamekuwa katika Uwepo wa Mungu, nao wanajua ya kwamba Yeye yuko. Ikiwa ni kwa ushindi au kushindwa, bado wanasimama vile vile. Hayo ndiyo aina ya mafunzo ambayo Mungu huwapa wanadamu. Na ni ajabu sana kuwazia ya kwamba Mungu angefanya hivyo, ya kwamba Mungu huwafunza watu Wake namna hiyo, bali Yeye hufanya hivyo. Mnajua, tuna wimbo wa kale tunaoimba:

> Wengine kupitia majini, wengine kupitia mafuriko,
> Wengine kupitia majaribu mazito, lakini wote kupitia Damu.

34 Mungu huwaongoza watu Wake kupitia majaribu makuu, kuwatakasa. Na wakati mwingine inachukua miaka kufanya hivyo. Na kwangu mimi, usiku wa leo, ninaamini kwamba sasa hivi Mungu anawafundisha watu kama hao kukabiliana na mstari wa mbele wa vita, watu wanaopitia, na, wakati, wanatetemeka kuanzia miguuni. Wakati mwingine inaonekana kana kwamba hicho kitu chote kinaanguka, lakini hata hivyo, katikati ya hayo yote, wanamjua huyo Mungu aliye hai na wanauelekeza uso wao mbele, wanazidi kwenda mbele.

35 Na watu wengi wanaombea uamsho, nashangaa kama hao wakati mwingine, kama hao wanaoomba, kama maombi yao wenyewe hayavizui visima vya baraka. Wakati wao ni waoga na wanaogopa kumwamini Mungu, wanahofia kuliamini Neno

Lake, wanaogopa kuamini ya kwamba Yeye angali hai leo, wakati Biblia Yake inaposema waziwazi, kwamba, “Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.”

36 Mungu hawaiti, kwa nadra sana, watu werevu, wenye elimu, wenye akili. Wana jukumu lao, na wao ni watu mashuhuri. Lakini kwa kawaida Mungu anapotaka kazi ifanywe, Yeye humchukua mtu ambaye karibu hajui ABC zake. Yachunguzeni Maandiko. Tafuteni kote katika historia. Watu waliotokea kuwa kitu fulani kwa Mungu hawakuwa watu ambao walikuwa na elimu kubwa, lakini ni watu ambao, vema, hawakuwa na elimu, nia tu moyoni mwao ya kumtumikia Mungu. Alimchukua mkulima, mchunga kondoo, mvuvi, mwindaji, wale walioishi katika maumbile. Katika utulivu huo na unyamavu wa maumbile, humo Mungu angeweza kuzungumza nao. Nao hao ndio aliowaita.

37 Na wakikuta kwamba, anapotoa wito kwa mwenye akili nyingi, mtu huyo hatimaye hurudi kwenye dhana zake za kiakili. Ndipo baada ya kitambo kidogo, inapofikia kutenda kazi za ajabu sana, amechanganyikana sana na walimwengu, asingeweza kukubali hizo. Kwa hiyo, hatimaye anaishia kwenye dhehebu, naye anapotoka na kufanyika mhudumu. Na hiyo ni sawa, wala sina neno dhidi ya mtu huyo ambaye angefanya hivyo.

38 Lakini Mungu anapokuwa tayari kufanya jambo fulani katika milki za kimbinguni Yeye kwa kawaida humchukua mtu ambaye anaweza kuweka tumaini Lake ndani yake, kisha anamtia mafuta na kumtuma huko nje, naye hana woga kazini. Hao ndio aina ya watu tunaowahitaji siku hizi; sio wasomi walioadibishwa, bali watu wanaomjua Mungu katika Nguvu za kufufuka Kwake.

39 Kwa mfano, kulikuwako na mtu katika Biblia, jina lake Musa, ambaye alikuwa amepata mafunzo yake yote. Alijua theolojia yote. Alijua kila kitu ambacho alipaswa kujua. Yeye . . . Kama angehitaji elimu yoyote, angeweza kuwafundisha mabingwa katika Israeli, au, katika Misri. Hakuhitaji kitu kimoja. Nayo Biblia inatwambia kwamba alifundishwa katika hekima yote ya Wamisri. Mbona, angeweza kuwafundisha wasomi wao. Angeweza kuwafundisha wanasayansi wao, mambo. Alikuwa bingwa hodari sana, inapokuja suala la kiakili. Lakini, hata hivyo, ilimchukua Mungu miaka arobaini kuyatoa hayo yote ndani yake, huko nje kwenye mchanga. Basi alipotolewa dhana zake zote za kiakili kuhusu Mungu, huko nje kwenye mchanga, hicho chuma kilikuwa tayari kufinyangwa.

40 Hivyo ndivyo Mungu huwachukua watu Wake na kuwaondolea woga wao wote na elimu yao yote, ndipo basi yule Mfinyanzi Mkuu anawaweka kwenye gurudumu na kuanza kuwafinyanga tena. Wafanyakazi, wastahilifu! Ni mtu wa

Mungu. Ni nani angeweza kumfundisha mtu zaidi ya Mungu Mwenyewe? Angalieni jinsi Yeye anavyowafunza.

41 Tungefikiria tena juu ya mwingine, jina lake Daudi. Mungu alikuwa akimfundisha Daudi alipokuwa mvulana mdogo tu. Nabii Samweli alipanda akammiminia mafuta kichwani, na kumtia mafuta, kwa sababu Mungu alikuwa akitaka kumfundisha Daudi kuwa shujaa hodari. Basi angalieni mafunzo aliyompa.

42 Nilikuwa nikisoma, siku moja, hapa kule Green's Mill, ambapo kwa kawaida mimi huenda kuombea, ambapo Mungu alimwambia Daudi, "Nimekutoa kwenye zizi la kondoo, kutoka kuwafuata hao kondoo wachache wa baba yako huko nje, nami nikakufanyia jina kuu kama wakuu wa dunia."

43 Nami nawazia mafunzo magumu aliyompa Daudi. Hakumsomesha hata kidogo katika shule fulani, bali alimsomesha katika shule Yake Mwenyewe. Daudi alikuwa mwindaji na mchunga kondoo. Na katika Zaburi aliandika juu ya malisho ya majani mabichi na maji matulivu, kwa sababu hapo alikuwa peke yake, mwenyewe. Hakuchafuliwa na mambo ya ulimwengu.

44 Mungu hana budi kumwondoa mtu kutoka katika mambo ya ulimwengu, ili Yeye aweze kumtuliza, apate kumsikiliza Mungu, ile Sauti ndogo, tulivu. Kisha, mara tu anapokutana na Mungu, anakuwa hana woga basi. Angalia kwamba hajali mtu yeyote anasema nini; amekuwa katika Uwepo wa Mungu. Anamjua Mungu katika Nguvu za kufufuka Kwake.

45 Halafu basi, Daudi, tunamwona. Siku moja, Mungu alimruhusu dubu aingie na kumkamata mmoja wa kondoo wake. Daudi akamfuatilia dubu huyo tu. Bila shaka aliomba, kwa sababu baadaye kidogo alikiri hilo. Naye akasali na kumwomba Mungu. Alikuwa mlinzi wa huyo kondoo. Hangeweza kumpoteza huyo kondoo. Naye hana budi kumwokoa huyo kondoo, kwa vyovyote vile. Basi akanyakua kombeo lake dogo, na kumfuatilia dubu huyo na kumwua. Hana budi kumwokoa kondoo huyo. Mnaona ni kwa sababu gani Mungu alikuwa akimfundisha?

46 Mungu anawataka wachungaji Wake wawaokoe kondoo, bila kujali inavyomlazimu kuitwa na yale yanayombidi kupitia. Waokoe hao kondoo!

47 Ndipo akaona ya kwamba Daudi alikuwa hodari juu ya dubu huyu, kwa hiyo alipandisha tu nguvu za huyo mnyama kidogo, ndipo akamtuma mwana-kondoo...simba kuingia akamkamata mmoja wa wana-kondoo.

48 Naye simba ni mnyama mkali. Loo, huko Afrika, nilipokuwa nikiwawinda...Simba anaweza kuwaua watu kumi kabla hujaweza kusema, "Jack Robinson." Loo, mnyama mkubwa mno, mwenye nguvu! Kwa mngurumo mkubwa tu na, ninii tu, watu wanaliwa. Naye anayekufa chini ya nguvu za simba kamwe

hasikii maumivu yoyote. Inatisha sana, kusikia mngurumo huo anaotoa. Miguu hiyo mikubwa mno, katika sekunde moja tu, amewararua watu dazani moja.

49 Na kuwazia, juu ya mvulana mdogo! Biblia ilisema alikuwa "mwekundu." Hiyo ina maana kwamba alikuwa. . .maskini jamaa mdogo tu, akiwa na kombeo dogo. Unajua ni kitu gani, kipande kidogo cha ngozi na kamba pande zote mbili. Na simba mwenye njaa, akiwa tayari ana ladha ya damu kinywani mwake, alikimbia na kumkamata kondoo. Daudi akamtumainia Mungu, na kusema, "Siwezi kumpoteza huyo. Wewe nisaidie, Bwana." Naye akamwangusha huyo simba chini, kwa kombeo. Ndipo huyo simba alipoinuka dhidi yake, mvulana huyo mdogo, naye simba akiwa na uzito wa kama ratili mia tano, ama zaidi, maskini mvulana huyo mwenye uzito wa labda sabini au themanini. Alichomoa, kutoka kwenye mkanda wake mdogo, kisu. Ndipo simba alipoinuka, ambaye angeua watu kumi kwa makofi machache, alimshika huyo simba ndevuni na kumwua.

50 Ujasiri! Mungu hataki waoga. Hawezi kukutumia kama unaogopa kulichukua Neno Lake na kumwamini Yeye. Anataka mashujaa, wasiozingatia chochote ila kile ambacho Bwana anasema. Hao ndio watu hana budi kutembea nao. Bila kujali kanisa linasema nini, mchungaji anasema nini, kile kanisa linachotetea; anamtetea Mungu na haki, na Neno Lake. Hao ndio watu tunaoninii. . .Mungu atakaowatuma siku hizi kwa ajili ya uamsho ambao watu Wake wanaombea.

51 Baadaye katika miaka, alipopanda kwenda kukutana na ndugu zake vitani, kulikuwako na jitu kubwa kule juu, vidole vya inchi kumi na nne. Naye akajigamba, na kusema, "Sasa acha mtu aje akapigane nami. Ikiwa unaweza kunipiga, nitajisalimisha, na vinginevyo, na tutatumika." Yeyote anayejisalimisha, bila shaka, atakuwa ndiye atakayeshindwa.

52 Hivyo ndivyo ibilisi anavyopenda kufanya. Anapofikiria kuwa anaweza kukushinda, atakwambia, "Huwezi kufanikiwa kwa hilo. Huwezi kuhubiri uponyaji wa Kiungu katika kanisa la Methodisti, kanisa la Baptisti." Vema, ninyi wahubiri wa Kimethodisti mshikeni tu Mungu wakati mmoja, mwone kama mnaweza ama hamwezi. Uh-huh. Kamwe hamtaweza kulifanya kwa theolojia yenu wanayofundisha. Itawabidi kumshika Mungu na kujua kwamba Yeye yuko.

53 Wanasema, "Wapentekoste." Miaka michache iliyopita, kulikuwako na kundi la watu waliosimama pembeni, hawana hata je—jengo wangaliweza kuingia. Lakini je, mlisoma gazeti la *Life*, hivi majuzi, yale waliyosema kuwahusu? Ni mojawapo ya matukio makubwa mno wakati huu uliowahi kujua, ni kule kuibuka kwa kanisa la Kipentekoste. Bila shaka. "Nao wanapata waongofu wengi zaidi katika mwaka mmoja kuliko makanisa mengine yote yapatavyo, yakijumuishwa pamoja."

Hivyo ndivyo gazeti la *Life* lilivyosema. Kwa nini? Huenda ikawa wamechanganyikiwa katika mambo fulani, lakini, ndugu, wao ni mashujaa; wanasimama huko nje, tayari kwa makabiliano, na kuita nyeusi "nyeusi" na nyeupe "nyeupe." Wakati hatimaye uamsho utakapoanza, utaanza miongoni mwao. Angalieni muone kama hautaanza. Watanyooshwa kabisa, moja ya siku hizi.

54 Basi, Daudi. Sauli alipomvika silaha zake, na kusema, "Daudi, ikiwa utapigana na jitu hili," kasema, "mbona, wewe si kitu ila mvulana, kijana tu, naye amekuwa askari wa vita tangu ujana wake, unawezaje kupigana naye?"

55 Msikilize huyu mtoto Daudi. Mnaona, hakusema hivi, "Sauli, mheshimiwa, bwana. Baba yangu alinipeleka shule ya sekondari, chuoni, shule ya upili. Nina Ph.D. Ni—ni—nimeandaliwa kufanya hivi. Mimi ni mtu mwenye akili." Kamwe hakusema hivyo.

56 Alisema, "Bwana wangu," akasema, "nilipokuwa nikichunga kondoo za baba yangu huko nje, dubu aliingia na kumkamata mmoja, nami nikamwua. Kisha simba akaingia na kumkamata mmoja, nami nikambwaga chini. Ndipo alipoinuka, nikamwua." Basi akasema, "Mungu aliyeniokoa na makucha ya dubu na simba, anaweza pia kuniokoa na mikono ya Mfilisti yule asiyetahiriwa." Mtu aliyefunzwa na Mungu!

57 Huyo hapo Sauli amesimama na mafunzo yote ambayo mtu yeyote angeweza kuwa nayo, kujua jinsi ya kupigana. Daudi hakujua lolote kuhusu upanga. Hakujua lolote kuhusu ngao. Vema, Sauli alienda na kumvika silaha zake kubwa mno, huku maskini mtoto Daudi alikuwa amesimama karibu ana matege. Wakagundua kwamba vazi lake la kikasisi halikumwenea mtu wa Mungu; lilimpondelea chini tu. Nazo kanuni zetu zote za imani na kadhalika hazitalingana na vifaa vya Mungu huko ng'ambo.

58 Loo, jinsi tungeweza kuendelea mbele zaidi na zaidi, na kuwataja wengi, juu ya wengi mbalimbali. Lakini, moja kwa moja kwenye fungu letu, kuharakisha.

59 Eliya alikuwa anazeeka, naye alijua kwamba haingechukua muda mrefu kabla haijamlazimu kuondoka ulimwenguni. Naye Mungu alikuwa amempata mtu ambaye alikuwa ni mtu mwaminifu, aliyekuwa mtu mwema. Jina lake lilikuwa Elisha. Sasa, iwapo mtaangalia, jina la mmoja wao ni Eliya na huyo mwingine ni Elisha.

60 Sasa, yeye kamwe hakuingia kwenye taratibu, na kadhalika, na kwenda na kuanzisha shule za theolojia, na huko katika shule kuu za upili za siku hizo. Alifanya nini? Alienda huko nje kondeni akamkuta mtu akilima na nira kumi na mbili za ng'ombe. Ati nini? Elisha, yule aliyekuwa akilima, alijua jinsi ya kuthamini safu nyoofu. Naye alijua kama angegeuka kutazama nyuma, angegaagaa atoke barabarani. Naye Mungu alijua ya

kwamba mtu aliyejua kulima mtaro mnyofu, alijua hapaswi kutia mikono yake kulima na hata kugeuka kuangalia nyuma. Kamwe hakungojea mpaka akapata elimu yake, akagaagaa barabarani. Alimchinja tu maksai na kutoa dhabihu, kisha akaondoka pamoja na Eliya, mara hilo vazi lilipowekwa juu yake. Alikuwa tayari, amejitolea. Mungu alijua angeweza kumwezesha.

61 Sasa, Mungu hana budi kumpa mafunzo fulani. Alikuwa akijifunza jinsi ya kuweka macho yake kwenye mtaro, na nira kumi na mbili za ng'ombe, na mtu mmoja akilima nazo. Alimfundisha subira, na jinsi ya kuwa mvumilivu, na kuwafundisha ng'ombe hao kutembea sambamba mstarini.

62 Ilimbidi kuwafunza baadhi ya watu, baadaye; kuwaweka kwenye Biblia, kwenye Neno, wakiwa vizuri na Mungu, kukaa sambamba mstarini.

63 Na, basi, hata Mungu ilimbidi kumfundisha kidogo. Akasema, "Sasa wewe kaa hapa, kwa maana ninaenda m—mpaka Gilgali. Bwana ameniita."

64 Naye huyo nabii, baada ya kuhisi hizo Nguvu juu yake, vazi hilo la Eliya, akasema, "Kama Bwana aishivyo, na roho yako iishivyo, sitakuacha."

65 Wakaendelea mbele mpaka Gilgali, ambao ni ma—mahali pa maungamo na ubatizo wa Kikristo. Kisha akasema, "Kaa tu hapa sasa. Hili ni zuri vya kutosha. Umefanya maungamo na ubatizo. Hapa ni pazuri vya kutosha. Ninapanda kwenda *Betheli*," ambao unamaanisha, "nyumba ya Mungu."

66 Sasa, huo ungekuwa sawa kwa watangaza imani wengi. "Loo, nimekuja hivi punde kanisani na kufanya ushirika. Kwa nini nisikae tu hapa?"

67 Lakini, sikilizeni, Elisha asingeweza kuwazia hivyo. Tayari alikuwa amehisi Nguvu za Mungu. Alijua kulikuwa na mengi zaidi kwa ajili yake. Kwa hiyo akasema, "Kama Bwana aishivyo, na nafsi yako iishivyo, sitakuacha." Loo, jinsi ninavyopenda hilo!

68 Ndipo akaenda mpaka kule, Betheli, kwenye nyumba ya Mungu, na huko akakuta kundi la wasomi. Wote walikuwa wahubiri waliofunzwa vyema, nao wakazunguka na kumwambia, wakasema, "Bwana, unajua nini? Uko nchani mwa fimbo. Je, ulijua kwamba Eliya ataondolewa kwako? Yeye ni mzee sana. Hawezi kuishi muda mrefu sana. Eliya ataondolewa, nawe utakuwa umesimama kule nje kama mlokole."

69 Hebu niwaambie jambo fulani sasa. Mtu ambaye amewahi kumwonja Mungu, hatakubali, ama, hawezi kukata kiu yake kwenye birika la kujibunia. Hawezi kufanya hivyo. Huko, theolojia yao yote waliyokuwa nayo kule kwenye shule ya

manabii, isingeweza kukata kiu ya mtu huyo wa Mungu, ambaye alikuwa amemwonja Mungu.

70 Nao wakaendelea kumshawishi, “Loo, unapaswa kukaa hapa. Na, mbona, katika majuma sita tungeweza kukupa Ph.D yako. Na, unajua, haitachukua muda mrefu sana, kabla hujachukua miaka minne hivi ya mafunzo hapa, nasi tungeweza kukupa wewe haki ya kuhubiri. Unajua, kama ungethibitika kuwa sawa, tungekutuma huko nje katika dhehebu letu.” Hilo halitamridhisha mtu wa Mungu. “Tutakufundisha kuwa mhudumu, ikiwa tu utakaa pamoja nasi kama miaka minne au mitano hapa.”

71 Hakuwa na wakati wa upuuzi kama huo. Alikuwa akienda zake kwenye Chemchemi hiyo. Alikuwa amekwisha kupita hayo. Alikuwa tayari ameonja utamu wa Mbinguni nafsini mwake.

72 Naye akasema, “Unajua kiongozi wako ataondolewa?”

73 Basi sikilizeni alichosema. “Naam, najua. Lakini nyamazeni.” Kwa maneno mengine, “Msipoteze pumzi yenu. Msijaribu kuniambia kuhusu hilo. Msijaribu kuniambia ninachofanya. Ninajua niendako na nitakalo.”

74 Mungu, tupe watu kama hao, watu waliofunzwa na Mungu ambao hawajui kugaagaa *huku* na kugaagaa *kule*.

75 “Najua niendako. Wala msinizungumzie kuhusu hayo. Nyamazeni tu. Msijaribu kunivunja moyo, kwa sababu haitafaa kitu.”

76 Loo, laiti watu walioombewa wangekuwa na ujasiri mwingi hivyo!

77 “Loo, siku za miujiza zimepita. Hiyo haikuwa halisi. Kuwa mwangalifu, utakuwa mgonjwa tena.”

78 “Nyamaza tu. Usiniambie chochote kuhusu hilo. Ninaendelea mbele. Uamsho unakuja. Mungu ameuahidi.” Loo, enyi wana wa Mungu, jongeeni kwenye mazingira yale huko ng’ambo, bila woga. Bila hofu! Liaminini Neno Lake Mungu.

79 “Najua a—ataondolewa. Lakini hilo silo ninaloninii... Hamna chochote hapa cha kunivutia. Digrii zenu zote na ma-Ph.D., na Shahada ya Sanaa, na upuuzi huu wote, hauniridhishi. Nyamazeni tu.”

“Naam, utaingia kichaa huko nje.”

80 “Kweli, kama nikiingia kichaa, acha niingie kichaa. Niko safarini.” Moja kwa moja, alikuwa anaenda.

“Huwezi kuufanya uvuke.”

81 “Najua siwezi kuuvuka, lakini Mungu atanivusha,” akasema.

“Vema, Elisha anaenda Yordani.”

“Ninaenda pamoja naye.”

Mungu anahitaji Yordani katika kila maisha.

82 Kwa hiyo, Elisha akakaribia. Kasema, “Sasa, Elisha . . .” Eliya akamwambia Elisha, “Wewe ni kijana tu,” labda kitu kama hiki, “na kwa kweli huna elimu yoyote.” Huyo nabii mzee alikuwa akijaribu kumpima. Akasema, “Wewe ni kijana tu. Hujasoma sana. Mbona, hujaninii . . . Ni, kwa kweli, huna elimu ya shule ya sekondari. Kitu pekee ujuacho ni kulima. Kwa hivyo ni afadhali ukae hapa, na huenda ukapata Shahada yako ya Sanaa. Unaona? Afadhali ukae ukapate digrii yako.”

83 Lakini si Elisha, sio mtu huyo ambaye wakati mmoja alikuwa amemgusa Mungu, akahisi Nguvu hizo za upako juu yake. Akasema, “Kama Bwana aishivyo, na nafsi yako isivyokufa kamwe, sitakuacha.” Alikuwa na kusudi. Aliona ono. Alijua kitakachotukia.

84 Nao wote wawili wakashuka kwenda Yordani. *Yordani* maana yake ni “mauti.” Hao hapo wamesimama, mzee na kijana. Hakika inamwakilisha Kristo pamoja na Kanisa Lake. Basi hao hapo wamesimama, kando ya Yordani. Huyo hapo, akishuka kutoka kwenye vilima vya Uyahudi, yale maporomoko makubwa yakinguruma namna hiyo. Naye Elisha, huku nywele zake zenye mvi zikining’inia mgongoni mwake, huku maskini macho yake yaliyofifia yakitazama ng’ambo ya Yordani . . . Naye yule kijana akitazama kila hatua aliyopiga. Mmoja, huyo kijana, alikuwa akingojea ono, apate kutekeleza mapenzi ya Mungu. Huyo mwingine alikuwa anaenda Nyumbani. Wote wawili walikuwa kwenye Yordani. Elisha, kwake . . . Anaenda Nyumbani.

85 Elisha alikuwa na maisha machungu. Huyo mhubiri mwanamke kule chini alikuwa amempitishia njia ngumu, Yezebeli na Ahabu. Na mawe na yote aliyokuwa ameyapitia! Elisha alikuwa anachoka. Naye alijua kwamba alikuwa amevipiga vita vilivyo vizuri, na mwendo alikuwa ameumaliza. Ng’ambo ya Yordani ndipo kustaafu kwake kulipokuwa.

Lakini Elisha alikuwa akiingojea Roho hiyo aliyokuwa juu yake.

86 Kwa hiyo, kama mkiangalia, kila mwaminio, unapofikia mahali ambapo inakubidi kujisalimisha, utahisi mawimbi baridi ya Yordani yakipigapiga miguuni mwako. Unavuka, au huvuki? *Yordani* ni “utengano,” kutenganisha.

87 Basi nyuma juu ya kilima walisimama wahubiri hawa, bado, wakimpigia Elisha makelele, “Afadhali usivuke. Utakiuka mpaka.” Mngali mnayasikia, hayo matamshi, bado, siku hizi.

88 Vema, Elisha akasema, “Kama Mungu ni Mungu, na huyo ni nabii Wake, sina budi kupachukua mahali pake, na ninahitaji roho yake kulitekeleza, sihitaji shule yao. Kama shule yao ingeweza kulitekeleza, wangekuwa wakipachukua mahali pake. Lakini Mungu aliniita kufanya hivyo, nami ninahitaji roho yake.”

89 Kama shule za makanisa zingalipachukua mahali hapo, na Nguvu ambazo Yesu alitoa, wangepachukua, miaka kadhaa iliyopita; Methodisti, Baptisti, Katoliki, Presbiteri. Lakini hazitafanya hivyo kamwe.

90 Inahitaji Roho wa Yesu Kristo! Nawe utauvuka Yordani, wa kila madhehebu nyuma yake, kila kitu kingine, na kusimama peke yako pamoja na Mungu.

91 Kwa hiyo, akasimama pamoja naye pale Yordani. Elisha akiangalia kule juu, akijua, mahali fulani huko ng'ambo, Mungu angemlaki. Basi akavua vazi lake, kisha akageuka akamwangalia huyo kijana. Ndipo akaupiga Yordani. Na alipofanya hivyo, Yordani ukafunguka. Nao wakatembea wakavuka, juu ya nchi kavu.

92 Mnaona, Yordani si mbaya sana, hata hivyo, kama una kitu Fulani cha kuifungua njia.

93 Loo, walipofika ng'ambo ya pili! Kwenye kila kichaka amefungwa farasi na gari. Mfalme wa wafalme alikuwa amewatuma wasindikizaji kumpandisha Eliya Nyumbani. Yote yalikuwa yamekwisha, kwa Eliya. Alikuwa ametosheka nayo, yapata miaka themanini na kitu, ya kuzozana na hao watu huko chini, na kulazimika. . . kupitia njaa na ugomvi, na kadhalika. Alikuwa tayari kwenda Nyumbani. Naye akageuka akamwangalia Elisha.

94 Naye Elisha alitaka kuona ono. Loo, alikuwa na masomo yote, huko nyuma ambako angaliweza kusimamia. Hawakuwa wakifikia popote. Mungu alikuwa anataka kumfundisha kwa njia Yake mwenyewe. Kwa hiyo alipoangalia kule, alipoangalia, vichaka hivyo vyo—vyote walimofungiwa mle, magari haya ya Moto na farasi wa Moto, vilimfanyia Elisha jambo fulani. Aliona ono. Ndiyo, ndugu!

95 Ndipo Mungu alipompeleka Eliya juu, alirudi na sehemu maradufu ya Roho wake. Alikuwa tayari kwa ajili ya uamsho basi.

96 Angalia mtu huyo basi, akiwa mvulana mkulima tu hapo awali. Mungu alilifanya jina lake lisiweze kusahaulika. Manabii wote waliosimama hapo karibu, wakimwangalia, iliwabidi kuinamia miguuni pake kwa sababu alikuwa na Nguvu za Mungu juu yake.

97 Wakati unakuja ambapo Mungu ataufanya ulimwengu kuinama miguuni pa wanaume na wanawake ambao wamejitosa na kuvuka Yordani, na kuyatenganisha mambo hayo. . . wenyewe, na mambo ya ulimwengu. Ndugu na dada, usiku wa leo, chochote ufanyacho, chochote unachowazia, vuka Yordani pamoja na Mungu. Vuka ukajitenge, acha ulimwengu nyuma. Acha Mungu akufundishe kwa ajili ya huduma Yake mwenyewe. Tunaishi katika siku moja kabla ya uamsho huu, lakini Mungu anachunguza, akijaribu kutafuta mioyo.

98 Angalieni. Alimpata mtu jina lake Paulo, loo, Mfarisayo mwenye ubinafsi. Lakini ilimbidi amshughulikie kabisa, kitu kama hicho, kabla hajaweza kuwa mwanafunzi. Angalieni yale aliyowafanyia watu, kote katika nyakati. Ilimbidi kuwachukua na kuivuta theolojia yao kutoka kwao. Naye Paulo, mara alipoona lile ono, hakupanda kwenda Yerusalemu, kwa Gamalieli, yule mwalimu mashuhuri, aliye mkuu kuliko wote Israeli, ambaye alikuwa amefundishwa naye. Hakumrudia kamwe, kumtaka shauri. Mbona, hata hakwenda Yerusalemu, kwa muda wa miaka kumi na minne baadaye. Lakini alishuka mpaka Misri, katika mkutano wa maombi. Na huko Mungu akamjalia kuandika Vitabu vingi vya Agano Jipya. Mnaona? Mungu anawatafuta watu. Alikuwa na mtu ambaye alimtaka aandike Agano hilo, kwa hiyo akamchagua tu Paulo. Naye akamtoa tu theolojia yake yote. Naye Paulo akasema ilimbidi kusahau yote aliyopata kujua, apate kumjua Kristo.

99 Mungu siku hizi anajaribu kutuondolea ulimwengu kwetu, na kutufanya tujifanye tupu, na tuwe wanaume na wanawake shupavu wanaompenda Mungu, na watakaodumu pamoja na Mungu, na watakaovuka mstari wa utengano, Yordani, ili Yeye aweze kututumia kwa ajili ya utukufu Wake.

100 Hii ndiyo saa ambayo nataka mfikirie sana. Na kama hujawahi kuvuka mahali hapa, kama hujawahi kuvuka mstari huu, ambapo ungali unasema, "Vema, mama yangu alikuwa mfuasi wa kanisa fulani." Hiyo ni sawa. Hiyo haipachukui mahali pako. Unaona?

101 Mungu anawaita wanaume na wanawake, leo hii, kwenye mstari wa mbele wa vita. Yeye hawaiti waende Gilgali, wala hawaiti waende Yeriko, au Betheli. Yeye ananinii... Wataangamia. Lakini anawaita wavuke Yordani, apate kukuingiza kwenye shule ya Nguvu Zake Mwenyewe, na kukufanya na kukufinyanga.

102 Angalieni yale anayofanya papa hapa sasa, kumtuma Roho wa Mwanawe. Anafanya ishara na maajabu na miujiza, ambayo ulimwengu haujayaona miaka elfu mbili iliyopita. Ulimwengu wa kisayansi umepiga picha Yake, ile Nguzo ya Moto, Malaika wa Bwana. Inaning'inia kule Washington, DC, usiku wa leo, kwenye ukumbi wa sanaa za kidini, Kiumbe pekee cha kimbinguni kilichowahi kuthibitishwa kisayansi kimepigwa picha. Anaonyesha ishara na maajabu yale yale Yake.

103 Ni kitu gani? Ni kuvuka Yordani. Kaa peke yako pamoja na Mungu. Kaa katika tanuru Yake Mwenyewe ya kusafishia. Ingia kwenye lile gurudumu kuu la Mfinyanzi Mkuu na umwache akufinyange. Usiku wa leo, wakati tukiwa katika maombi, wakati tunapokuja mahali hapo, jilaze mwenyewe moja kwa moja kwenye gurudumu Lake, na kusema, "Bwana, mimi hapa.

Nifinyange na unifanye kwa mtindo Wako Mwenyewe." Naye Mungu atafanya hivyo.

104 Tunapoinamisha vichwa vyetu kwa muda kidogo tu kwa maombi mafupi. Kabla tu ya maombi, ningependa kuwauliza watu walio ndani na nje swali hili. Ni wangapi humu ndani kwa uaminifu wangependa kwenda pamoja na Yesu huko Yordani, usiku wa leo, na huko uvuke kule ambako ungeweza kuona ono na kuona kile ambacho Mungu anamaanisha hasa? Mwaweza kuinua mikono yenu? Mungu awabariki. Angalieni tu! Nadhani kuna mikono mia mbili jengoni, iliyoinuliwa. Shuka uende Yordani, si kushuka kwenye seminari. Elisha aliipita hiyo moja kwa moja.

Wakasema, "Ngojea hapa."

105 Akasema, "Sitaki. Hiyo ni ya kujibunia." Ah, haitakata kiu hiyo ya mtu ambaye ana kiu kwa ajili ya Mungu. Hakuna ujuzi wa seminari, hakuna—hakuna digrii za sanaa, au kadhalika, kamwe, kamwe hazitazima kiu hiyo, mpaka umeinywea Chemchemi hiyo ya Uzima.

Ninyi mlioinua mikono yenu, ombeni pamoja nami sasa.

106 Mungu Mpendwa, katika dakika hizi chache za ibada, huku wanaume na wanawake wakisimama kando ya kuta, wavulana kwa wasichana; na upande wa nje, wakiegemea madirishani; joto. Lakini hata hivyo kuna kitu ndani yao, kwamba Wewe umevutia usikivu wao, la sivyo wangeondoka. Wasingesimama hapo namna hivyo.

107 Bwana Mungu, kwa sababu wanajua ya kwamba wao ni wanadamu tu. Nasi tulisoma gazetini ambapo mmoja wa waheshimiwa mameya wetu wastaafu alimsikiliza Makamu wa Rais akizungumza, akaondolewa. Mwingine kwenye mchezo wa mpira, hivi majuzi usiku, mtu mashuhuri, aliondoka upesi. Nazo nafsi zao ziko mahali fulani usiku wa leo. Mungu, hiyo itakuwa ndiyo njia yetu siku moja. Labda sio kwa njia ile ile, lakini hatuna budi kuondoka.

108 Basi jalia watu wajirudie na watambue ya kwamba kuwa mfuasi wa kanisa tu sicho kile unachohitaji. Unataka watu wajazwe na Roho, wazaliwe, wachongwe, wachomwe kwa Roho Mtakatifu, wakapigwe chapa, watu ambao wamevuka mpaka, watu walioitwa na Mungu. Nasi tunaamini ya kwamba Wewe utatuma uamsho ambao Billy Graham na wengine wengi wanauombea. Unapoweza kuwatoa watu wawe peke yao, mbali na shule yao ya theolojia, mbali na njia zao za kibinafsi, watu shupavu, watu wenye—wenye tabia kama Yako, wanaokuamini na kuliamini Neno Lako.

109 Mungu, jalia wengi wao wasimame hapa sasa, ambao watamtolea Bwana Yesu yote waliyo nayo, na waachanane kabisa na ulimwengu, waende waupite Gilgali, mahali pa maungamo na chanzo cha Ukristo. Waende mbele kupita shule

ya manabii walioketi kule nyuma na theolojia yao. Waende mbele mpaka Yordani, kwenye ono wazi wakati watakapovuka, waone kwamba Mungu aliye hai angali anaishi.

110 Baadaye tunamwona nabii huyu akimtazama pande zote, na kulikuwa na Malaika wale wale wa Moto, na magari ya farasi, huko chini Dothani, siku moja.

111 Ungali hapa usiku wa leo, Bwana. Waite wanaume Wako, waite wanawake Wako, wavulana Wako, wasichana Wako, Bwana. Nena amani mioyoni mwao na uwajalie wavuke, kupita mambo ya ulimwengu. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu na kwa ajili Yake. Amina.

112 Ninataka kuimba huo kwa muda mfupi tu, kwa utulivu sana katika ibada.

> Fanya upendavyo, Bwana!
> Fanya upendavyo!
> Shikilia juu ya utu wangu
> Ushawishi mkamilifu!
> Niumbe na unifinyange
> Kulingana na mapenzi Yako,
> Wakati nikisubiri,
> Nimejitolea na ni mtulivu.

Sote pamoja sasa, katika njia ya ibada.

> Fanya upendavyo . . .

Sasa jiweke wakfu kwenye wimbo huo, kwa wimbo huo, kwa Mungu.

> Fanya upendavyo!
> Shikilia juu utu wangu
> Ushawishi mkamilifu!
> Niumbe na unifanyange
> Kulingana na mapenzi Yako,
> Wakati nikisubiri,
> Nimejitolea na ni mtulivu.

113 Kimya kimya sasa, katika kuabudu sasa. Usiangalie huku na huku, mwangalie Mungu tu.

> Fanya upendavyo . . .

Limaanishe kweli.

> Fanya upendavyo!
> Wewe ndiwe Mfinyanzi;
> Mimi ni towe.
> Niumbe na unifinyange
> Kulingana na mapenzi Yako,
> Wakati nikisubiri,
> Nimejitolea na ni mtulivu.

114 Ninaamini ingekuwa ni vema sana. Mnapenda kuabudu? Ujumbe umekwisha sasa. Hebu tuabudu tu, kwa dakika moja,

huku vichwa vyetu vimeinamishwa, wimbo huo tena. Umaanishe kutoka moyoni mwako.

Fanya upendavyo . . .
Fanya upendavyo!
Wewe ndiwe Mfinyanzi;
Mimi towe.
Niumbe na unifinyange
Kulingana na mapenzi Yako,
Wakati nikisubiri,
Nimejitolea na ni mtulivu.

115 Bwana, tujalie haya: Jalia kila mmoja, kuanzia watoto hawa wadogo hadi kwa mwanamume na mwanamke mkubwa zaidi katika Uwepo wa Kiungu, Roho Mtakatifu na afanye kazi sasa juu ya imani yao na kuondoa mashaka yao yote, maskini kushindwa kwote, na wafinyangwe kulingana na mapenzi Yako. Wakati wakiwa kwenye gurudumu Lako kuu la kufinyanga, tunaziweka nafsi zetu kwa ajili ya kuwekwa wakfu, kufinyangwa upya. Tujalie, Ee Mungu, katika Jina la Yesu, Mwanao. Amina.

116 Ninapenda tu hii. Nanyi je? Kimya tu tukimhisi Roho Mtakatifu. Loo, baada ya Ujumbe mkali, halafu huo utamu wa Roho Mtakatifu! Huja kwa Neno. Nitaimba mstari wa huo, au nitajaribu.

Inadondoka damu, naam, inadondoka damu,
Injili hii ya Roho Mtakatifu, inadondoka damu,
Damu ya wanafunzi waliokufa kwa ajili ya Kweli,
Injili hii ya Roho Mtakatifu inadondoka damu.

Wa kwanza kufa kwa ajili ya mpango huu wa Roho Mtakatifu,
Alikuwa Yohana Mbatizaji, lakini alikufa kama mwanamume;
Ndipo akaja Bwana Yesu, wakamsulubisha,
Alihubiri ya kwamba Roho angewaokoa watu kutoka dhambini.

Walikuwako Petro na Paulo, na Yohana mtauwa,
Waliyatoa maisha yao kusudi Injili hii ipate kuangaza;
Walichanganya damu yao, kama wale manabii wa kale,
Kusudi Neno la kweli la Mungu litangazwe kwa uaminifu.

Ndipo wakampiga Stefano mawe, alihubiri dhidi ya dhambi,
Aliwakasirisha sana, wakakiponda kichwa chake;

Lakini alikufa katika Roho, akakata roho,
Ndipo akaenda kujiunga na wale wengine, lile jeshi lililotoa uhai wao.

Nafsi zilizo chini ya madhabahu, zinalia, "Hata lini?"
Bwana apate kuwaadhibu wote waliotenda mabaya;
Lakini kutakuweko na wengine watakaotoa damu ya uhai wao,
Kwa ajili ya Injili hii ya Roho Mtakatifu na mafuriko Yake mekundu sana.

Sote pamoja sasa.

Inadondoka damu, naam, inadondoka damu,
Injili hii ya Roho Mtakatifu, inadondoka damu,
Damu ya wanafunzi waliokufa kwa ajili ya Kweli,
Injili hii ya Roho Mtakatifu inadondoka damu.

117 Walikuwa nini? Wanaume ambao Mungu aliwafundisha na kuwaita. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Mungu anawezaje kumtumia mwoga kuweka Neno Lake ndani yake? Yeye ni mwoga. Hiyo ndiyo sababu hawajui kitu juu Yake. Watu wasio na woga, ambao Mungu amewatahiri kwa Roho Mtakatifu, Mungu anaishi ndani. Yeye angeitia muhuri damu yake kuwa sivyo, ushuhuda wake kwa damu yake; haijali. Anamwishia Kristo. "Kwangu mimi kuishi ni Kristo, na kufa ni faida." Hivyo ndivyo walivyojisikia kuhusu hilo. Amina.

118 Sasa ni wakati wa mstari wa maombi. Na ni mstari wa maombi ya mapema, yapata tu saa mbili na dakika ishirini. Lakini tunataka kuwaombea watu. Nami nawatakeni sasa, hii . . . Mahubiri yote ambayo tungeweza kufanya yasingeweza—yasingeweza kulinganishwa na Neno moja lililonenwa kutoka kwa Mungu Mwenyewe.

119 Sasa ili kuanzisha mstari wa maombi, ambao, tuliahidi kuwaombea wote. Hilo tutafanya, Mungu akipenda. Sisi, kila usiku, tumesambaza kadi za maombi. Na kusema, katika hili, kwamba . . . Kila usiku tungeita kundi kutoka humo, kwa ajili ya utambuzi. Lakini watu, basi, baadhi yao wangeondoka usiku huo. Tungekuwa na mkutano mkuu, na Roho angeshuka, nao watu wangeondoka. Na kesho yake usiku ingetulazimu kusambaza zaidi.

120 Na ikiwa sijakosea, si ninamtazama Fannie Wilson amesimama pale nyuma? [Dada Wilson anasema, "Hiyo ni kweli."—Mh.] Nakumbuka nikimchukua mwanamke huyo, yapata kumi na saba . . . Loo, zaidi ya hiyo, kama ishirini- . . . ["1932."] 1932, akifa, kwa TB, naye daktari wa jiji hili alikuwa amemkatia tamaa. Naye alikuwa anatokwa damu mpaka mablanketi na kila kitu yalikuwa yamelowa damu. Mumewe

na bintiye walikuja na kunichukua, asubuhi moja. Nikaenda huko na kuitia juu yake, Jina la Bwana Yesu. Na yapata siku chache baadaye, katika majira ya baridi kali, nikambatiza kwa Jina la Bwana Yesu, mtoni. Naye akashuka barabarani, nyuma ya maskini lori la ng'ombe, amelowa maji kabisa. Angali hai usiku wa leo, kwa sababu Kristo alifanya jambo hilo. Mara ya kwanza kumwona baada ya miaka mingi. Nikiangalia kote juu ya kusanyiko, nikiliona.

121 Mungu angali hai. Hiyo ni kweli. Naye alisema, "Kwa kuwa Mimi ni hai, ninyi nanyi mnaweza kuishi pia."

122 Sasa ningependa, kwa namna fulani kuwaelezea kwamba hii ni nini, kwa sababu, nisipofanya hivyo, basi mnaweza kuondoka na kusema, "Vema, sielewi hilo."

123 Sasa, hoja zangu ni hizi, kwamba, "Yesu Kristo anabaki yeye yule jana, leo na hata milele." Sasa, kama Yeye ni yule yule, hana budi kuwa yule yule katika kila kanuni, yeye yule katika—katika nguvu, yeye yule katika uweza, yeye yule katika kila kitu alichokuwa.

124 Na wakati alipokuwa hapa duniani, kulikuwako na Wayunani fulani, wakati mmoja, ambao walikuja na kusema, "Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu."

125 Nami ninaamini ya kwamba hiyo ndiyo shauku ya kila mwanamume ama mwanamke aliyepata kusikia habari za Yesu, anataka kumwona. Na kama Yeye si yule yule, basi hatuwezi kumwona. Lakini iwapo Yeye ni yeye yule, tunaweza kumwona, la sivyo Yeye alisema uongo. "Bado kitambo kidogo, na ulimwengu hautaniona tena, bali ninyi mtaniona, kwa maana Mimi," kiwakilishi nafsi, "nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu hata ukamilifu wa dahari." Na ndipo Yesu akaahidi kuwa katika Kanisa Lake, akifanya mambo yale yale aliyofanya wakati huo, mpaka wakati uishe. Sasa, Yeye alisema, "Bado kitambo kidogo," ulimwengu hautamwona Yeye tena. Vema, basi, tungemwonaje? Inatubidi kumwona Roho Wake, kama Yeye yuko ndani yetu, basi Roho huyo ingembidi kufanya vile vile alivyofanya wakati huo, la sivyo asingekuwa ni Roho yeye yule.

126 "Mimi ndimi Mzabibu, ninyi ni matawi." Na endapo tutazaa... Iwapo tawi liko ndani ya Mzabibu, hilo tawi litazaa aina ya matunda ambayo Mzabibu unazaa. Vema, Mzabibu wa kwanza uliotokea... Tawi la kwanza lililotokea kwenye huo Mzabibu lilikuwa ni tawi la kipentekoste; maono, nguvu, uponyaji, ubatizo wa Roho Mtakatifu, ishara kuu na maajabu. Tawi linalofuata itabidi liwe tawi la aina ile ile. Moja kwa moja hadi mwisho, itabidi liwe vivyo hivyo. Hivyo ndivyo Yesu alivyosema.

127 Sasa, hebu tuone alivyokuwa jana. Kama tunaweza kuona kile alichokuwa jana... Sasa, ninachukua njia ya mkato, kwa sababu ya wakati; nitatoa kama dakika tano za mafunzo. Na

kama tunaweza kuona kile alichokuwa jana, basi tunaweza kuona kile alicho leo, na atakachokuwa milele. Je, hilo ni zuri vya kutosha?

128 Sasa, wakati alipokuwa hapa duniani, Yeye alikuja kama Masihi, akabatizwa na Yohana Mbatizaji; hakuwa ametenda kazi bado. Naye akaingia katika huduma Yake ya mwanzoni. Alitumwa kwa nani? Wayahudi.

129 Sasa, tunatambua kuna mataifa matatu tu ya watu ulimwenguni, hayo ni: Myahudi, Mmataifa, na Msamaria; ambao ni watu wa Hamu, Shemu, na wa Yafethi. Myahudi, Mmataifa, na Msamaria.

130 Mnakumbuka? Petro aliwatembelea, akiwa na funguo za Ufalme, kwenye Siku ya Pentekoste, kwa Wayahudi. "Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo."

131 Filipo akashuka na kuwahubiria Wasamaria. Wote wakaamini na kutubu, nao walikuwa wamebatizwa kwa Jina la Yesu Kristo. Ila, Roho Mtakatifu hakuwa amewajilia. Petro alikuwa na funguo. Akashuka na kuweka mikono juu yao, nao wakampokea Roho Mtakatifu.

132 Halafu Kornelio, yule Mmataifa, akaona ono, kwamba aagize mtu aitwaye Petro aitwe, Simoni Petro, ambaye aliishi katika nyumba ya mtu ambaye alikuwa mtengenezaji wa ngozi. Basi Petro alipofika huko, "Petro alipokuwa akisema Maneno haya, Roho Mtakatifu akawashukia." Ndipo Petro akasema, "Mtu anaweza kuzuia maji? Hawa wamempokea Roho Mtakatifu kama tulivyompokea hapo mwanzo." Kila tawi likichipuka vivyo hivyo. Mnaona?

133 Sasa, Yesu alipokutana . . . Sasa, Yeye hakuwajia Mataifa. Ni wangapi wanaojua hilo? Aliwakataza wanafunzi Wake kwenda kwa Wamataifa wowote. Ni wangapi wanaojua hilo? "Katika njia za Mataifa msiende, afadhali shikeni njia kuwaendea kondoo waliopotea wa Israeli. Na katika kuenenda kwenu, hubirini, mkisema, 'Ufalme wa Mbinguni umekaribia,' kwa kondoo waliopotea wa Israeli."

134 Sasa, ni nani waliokuwa wakimtazamia Yeye kuja katika siku hiyo? Si Mataifa; tulikuwa makafiri, Waanglo-Saksoni. Tulikuwa Warumi, tukiabudu jua na kadhalika. Hatukuwa tukimtazamia Masihi yeyote, bali Wayahudi na Wasamaria walikuwa wakimtazamia. Sasa je, Yeye alijitangazaje Mwenyewe kwa hao watu waliokuwa wakimtazamia?

135 Hebu turudi sasa kwa Yohana Mtakatifu, mlango wa kwanza, na kwa muda kidogo sasa. Basi sikiliza kwa makini.

136 Myahudi wa kwanza aliyepata kuletwa Kwake, wakati Filipo au . . . Andrea alipoongoka, kisha akaenda akakutana na ndugu yake, Simoni Petro, yeye alimleta Simoni mbele ya Yesu. Naye Yesu akamwambia jina lake lilikuwa nani, na baba yake alikuwa

nani. Ni wangapi wanaojua hilo? Unafikiri hilo lilifanya nini kwa mtu huyo, ambaye baadaye angekuwa na funguo za Ufalme mkononi mwake? Hivyo ndivyo alivyojithibitisha Mwenyewe kuwa, Masihi.

137 Haraka, basi, Filipo akaongoka, kisha akaenda akampata Nathanaeli. Hizo ni maili thelathini kuzunguka mlima. Basi akaja nyumbani, nami ninaweza kumsikia akisema, "Loo, Bibi Nathanaeli, yu wapi Nathanaeli?"

"Loo, yuko huko nje katika—katika shamba la mizeituni."

138 Akaenda huko mbio sana, "Nathanaeli, uko wapi?" Basi akamkuta chini ya mti. Naye Nathanaeli alikuwa akiomba. Naye akangoja mpaka akamaliza kuomba. Ndipo akasema, sio, "U hali gani, Nathanaeli? Je, mazao yanaendeleaje?" Loo, alikuwa na ujumbe! Ndivyo alivyo mtu ambaye amekutana na Yesu. Hana wakati wa ujinga. Akasema, "Njoo, umwone Yeye tuliyempata, Yesu wa Nazareti, mwana wa Yusufu!"

139 Na sasa ninaweza kumwona Nathanaeli akipangusa nguo zake, kutoka kwenye maombi. Akasema, "Sasa, Filipo, nimekujua kuwa mtu mwema, na mtu mwaminifu. Sasa, je, laweza neno lolote jema kutoka Nazareti? Vema, unajua, kama Masihi angekuja, Yeye angekuja Yerusalemu, kupitia kwa kanisa." Hivyo ndivyo watu wanavyofikiria siku hizi. Mnaona? "Angekuja kupitia Yerusalemu. Kayafa kamwe hakulitangaza kwenye ule mkutano wa mwisho. Kwa hiyo, hakuna hata mmoja wa wanatheolojia aliyelitangaza. Kwa hivyo nimekujua kuwa mtu mwaminifu. Kwani umeingia kichaa?"

"Loo, hapana. Wewe njoo ukajionee."

Akasema, "Laweza neno lolote jema . . . "

140 Akampa jibu zuri sana mtu yeyote angeliweza, akasema, "Njoo, ujionee mwenyewe."

141 Sasa, akienda zake njiani, ninaweza kumsikia Nathanaeli akisema . . . au Filipo akimwambia Nathanaeli, "Unajua nini? Unamkumbuka yule mvuvi mzee kule chini ambaye hakuweza hata kutia sahihi risiti ile ulipompa zile, uliponunua wale samaki kwake?"

"Naam. Ninaamini jina lake lilikuwa Simoni."

"Naam, ndivyo hivyo."

142 "Nilimleta, hivi majuzi, huko juu mbele ya Masihi huyo, na mara tu Yeye alipomwona, alisema, 'Jina lako ni Simoni. Jina la baba yako ni Yona.' Nami . . . Haitanishangaza, ila utakapokuja mbele Yake, kama Yeye hatakwambia wewe ni nani."

Akasema, "Ah, sasa, ngoja kidogo, si mimi."

143 Kwa hiyo, kesho yake wakawasili. Naye Yesu alikuwa kwenye mstari wa maombi, kama kawaida, akiwaombea wagonjwa, ndipo wakati Yeye, angaliweza kuja na kuingia

kwenye hilo kusanyiko, Yesu akaangalia juu, Naye akamwona Filipo akija, akimleta mtu kupitia kwenye marefu ya kanisa. Naye akamwangalia, akasema, "Tazama Mwisraeli ambaye hamna hila ndani yake."

144 Ati hilo ni Fundisho la kigeni? Huyo alikuwa ni Yesu, jana. Huyo ni Yesu, leo, iwapo Yeye ni yeye yule.

145 Ndipo huyo mtu akasimama. Ninaweza kumwona Nathanaeli, uh, Filipo akimgusa, kasema, "Nilikuambiaje? Nilikuambiaje?"

146 Akasema, "Rabi," maana yake ni *mwalimu*, ama chochote tunachoweza kumwita siku hizi, mwajua. Kwa kweli, neno sahihi la Kiebrania, linamaanisha *mwalimu*. Kasema, "Rabi, ulipata kuniona lini? Unajuaje chochote kunihusu? Sijawahi kukuona maishani mwangu. Unajuaje kwamba mimi ni Mwisraeli? Unajuaje kwamba mimi ni mwenye haki, na mwaminifu, na mkweli? Hujawahi kuniona, maishani Mwako. Umenitambuaje?"

147 Akasema, "Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikuona," maili thelathini kuuzunguka mlima, majuzi. Macho ya jinsi gani!

148 Sasa alisema nini? Alisema, "Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu. Wewe ni Mfalme wa Israeli." Ikiwa Wayahudi walitambua hilo... Sasa ngojeni. Huyo alikuwa ni Myahudi aliyeteuliwa. Ni wangapi wanaoamini katika uteule? Loo, kuna watu wengi ambao hawataupokea. Mnaona? Biblia ilisema hivyo. Lakini mtu huyo alikuwa na Roho wa Mungu ndani yake. Naye akakiri, akasema, "Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu. Wewe ni Mfalme wa Israeli."

149 Lakini hapo walisimama wanatheolojia wa siku hizo, makuhani na wale waalimu wakuu, wakimsikiliza. Nanyi mnajua walichosema? Walisema, "Yeye ni mpiga ramli. Ana roho ya Beelzebuli juu Yake." Yesu... Hawakulisema moja kwa moja, kwa sauti kuu. La, la.

150 Lakini Yesu akageuka na kuwaangalia. Akasema, "Mnaweza kuniita hivyo na kupita nalo. Lakini utakuja wakati ambapo Roho Mtakatifu atakuja, basi mtakaposema neno moja dhidi Yake akifanya jambo lile lile, kamwe halitasamehewa katika ulimwengu huu wala ulimwengu ujao."

151 Kwa hivyo basi tunashughulikia nini? Hao walikuwa ni Wayahudi. Wayahudi wa kweli kabisa na waaminifu walimwamini Yeye kuwa ndiye Masihi.

152 Waalimu na wanatheolojia, walikuwa nini? Uzao wa nyoka, kama tulivyopitia. Alisema, "Ninyi ni wa baba yenu, ibilisi." Hata hivyo, walikuwa watu werevu, wenye akili, watakatifu. Hawangelilisogeza jani... Watakatifu. Wasingeivunja Sabato. Wasingekula nyama zozote. Walikuwa watu watakatifu, lakini

wakashindwa kuona. Mnaona, walikuwa wamefunzwa na wanadamu.

Mungu huwafunza watu Wake, wagumu. Hiyo ni kweli. Watu walioitwa na Mungu!

153 Kisha siku moja Yeye—Yeye angeninii . . . Hivyo ndivyo Wayahudi walivyowazia. Hivyo ndivyo alivyojitambulisha Mwenyewe kwa Wayahudi. Ni wangapi wanaojua hayo ni Maandiko? Vema. Sasa, kama Yeye alijitambulisha kwa Wayahudi, huyo alikuwa ni Yesu jana pamoja na Wayahudi.

154 "Sasa, ulisema, 'Wasamaria walikuwa wakimtazamia Yeye kuja.'" Naam, walimtazamia, bali si Mataifa. Wasamaria tu.

155 Basi alipokutana na Wasamaria kwa mara ya kwanza, Yeye alikuwa hana budi kupitia Samaria. Naye akasimama, akawatuma wanafunzi Wake, kununua chakula, yapata saa sita. Akaketi kwenye kisima. Huyu hapa mwanamke anakuja, akaanza . . . Sasa, tunamjua, katika nchi hii, kuwa ni mwanamke mwenye sifa mbaya, mwanamke wa mtaani, mnajua, kahaba. Na kwa hiyo akatoka na kuanza kuteremsha ndoo kisimani, kuteka maji. Ndipo akasikia Sauti ikisema, "Mwanamke, nipe maji ninywe." Naye akatazama pande zote na huyu hapa ameketi Myahudi wa makamu.

156 Alikuwa tu wa miaka thelathini na kitu, lakini Biblia ilisema alionekana wa hamsini. Walisema, "Wewe ni Mtu hujapata umri wa miaka hamsini, na unasema kwamba Wewe 'umemwona Ibrahimu'?"

157 Akasema, "Ibrahimu asijakuwako, Mimi niko." Mnaona? Hapana shaka alionekana mzee kidogo kwa sababu ya kazi Yake, mwili Wake wa kibinadamu.

158 Naye akatazama pande zote. Alijua Yeye alikuwa Myahudi. Akasema, "Bwana, si kawaida kwenu Wayahudi kuwaomba Wasamaria mambo kama hayo. Hatuna uhusiano wowote sisi kwa sisi."

159 Akasema, "Mwanamke, kama ungalijua ni Nani unayesema Naye, ungeniomba Mimi maji unywe. Na ningekuletea, nikupe maji usije hapa kuteka." Alikuwa akifanya nini? Kuwasiliana na roho yake. Mnaona? Angalieni, atajitangaza Mwenyewe kwa Wasamaria, sasa.

160 Naye akasema, "Mbona, ninyi mnasema, 'Abuduni Yerusalemu.' Tunasema, 'Katika mlima huu.'"

161 Akasema, "Saa inakuja, na sasa ipo, ambapo hamtamwabudu Mungu, katika mlima huu wala kule Yerusalemu, bali katika Roho na Kweli. Baba anawatafuta watu kama hao."

162 Alikuwa akifanya nini? Kuishika roho yake. Basi baada ya kitambo kidogo, alipopata shida yake ilipokuwa . . . Ni wangapi wanaojua shida yake ilikuwa nini? Alikuwa na waume watano,

naye alikuwa akiishi na wa sita. Kwa hiyo, Yeye akasema, "Mwanamke, nenda kamwite mumeo mje naye hapa."

Akasema, "Sina mume yeyote."

163 Akasema, "Hiyo ni kweli. Unao...umekuwa na watano, naye unayeishi naye sasa siye wako."

164 Akasimama na kumtazama. Sasa, yeye hakusema, "Wewe ni Beelzebuli, bwana. Wewe ni mpiga ramli." Alijua zaidi juu ya Mungu kuliko nusu ya wahubiri wa Jeffersonville, hiyo ni kweli, akiwa ni kahaba. Akasema, "Bwana, naona ya kuwa Wewe ni nabii."

165 Tazama, "nabii." Na kama ukilifuatilia neno hilo huko nyuma, utaliona, yule Nabii ambaye Musa alisema angekuja, mnaona, "Bwana, Mungu wenu, atawaondokeshea Nabii kama nilivyo Mimi."

166 Akasema, "Naona ya kuwa Wewe ni nabii." Alijua Yeye hakujua hilo kwa njia nyingine yoyote; asingeweza kujua. Kasema, "Naona ya kuwa Wewe ni nabii." Sasa sikiliza hapa, "Sisi..." Wasamaria, sio Wayahudi sasa, Wasamaria, "Tunajua, Masihi ajapo, Yeye atatwambia mambo haya." Mnaona ni ishara ya aina gani waliyokuwa wakitafuta? Ile ishara ya Masihi. "Masihi ajapo, Yeye atatwambia mambo haya, lakini u nani Wewe?"

Akasema, "Mimi ninayesema nawe, Ndiye."

167 Naye akaangusha mtungi wake wa maji, akakimbilia mjini, na kusema, "Njoni, mwone Mtu aliyeniambia mambo niliyoyatenda. Je, haimkini huyu kuwa ndiye Masihi?"

168 Kama hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya Masihi wakati huo, haina budi kuwa ndiyo ishara ya Masihi siku hizi. Kama Yeye ni... Sasa, kumbukeni, hakuna wakati hata mmoja ambapo mwujiza huo uliwahi kufanywa mbele ya Mmataifa. Ilikatazwa. Kwa nini? Mataifa walikuwa na miaka elfu mbili ya mafundisho ya kanisa.

169 Lakini sasa mwisho wa kipindi cha wakati wa Mataifa umewadia. Nayo Urusi, wakomunisti, wana bomu lililoelekezwa moja kwa moja kwenu, kukimaliza, pia. Msijali, inakuja. Biblia ilisema hivyo. Itakuwa hapa huku jina lenu limeandikwa juu yake, nalo litageuka kuwa poda katika sekunde moja, taifa zima. Itakuwa maangamizi kabisa. Angalieni, huyo ni Mungu anayefanya hivyo. Ninajua wao ni wafalme huru, ni kundi la makafiri. Lakini je, Mungu hakuinua mataifa ya kikafiri kuinyoosha Israeli katika siku zilizopita? Biblia inadai kwamba Urusi na ukomunisti unatumika moja kwa moja mikononi mwa Mungu, kuwaondosha kabisa watu duniani.

170 Lakini kabla jambo hilo halijatukia, Unyakuo unakuja na kulipeleka Kanisa Nyumbani kabla jambo hilo halijatukia. Na kama hilo liko karibu jinsi hiyo, Unyakuo u karibu jinsi gani? Karibu kuliko hilo. Kwa hivyo mnaona ni kwa nini tuko...

kwa nini ninahubiri jinsi ninavyohubiri, kwa nini ninajitahidi kwa bidii niwezavyo; kwa nini Mungu ni kila kitu anachoweza kufanya, kushindilia hilo ndani ya Wateule, kuuvuta Uzao wa mwanamke utoke, kusudi uzao wa nyoka upate kuadhibiwa. Hilo ni kweli kabisa. Hilo ndilo aliloahidi kufanya.

171 Sasa, kama Yesu alijitangaza Mwenyewe mbele ya Myahudi na mbele ya Msamaria, kwa ishara hizo, kisha atatuacha twende bila kututangazia ishara iyo hiyo, Yeye ni dhalimu, kama akituacha tupite tu, kwa kusema, "Sisi ni Methodisti; sisi ni Baptisti; sisi ni Katoliki; sisi ni Presbiteri," la, bwana, kama Yeye akituacha tupite pamoja na theolojia baridi.

172 Hana budi kuja na ishara, maajabu, kama tu alivyofanya hapo kwanza, ikiwa Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Tumeifikia siku hiyo. Tuko hapa sasa. Kwa Biblia, kwa ushuhuda, kwa Roho, kwa sayansi, kila kitu kinathibitisha ya kwamba kiko hapa. Loo, mimi . . . Loo, laiti ningalikuwa na nguvu za kulisukuma hilo ndani ya watu, kuwafanya walione.

173 Ninyi watu hapa Jeffersonville ni watu wangu. Nimelelewa pamoja nanyi. Na mimi na—nawapenda. Msi—msiniwazie kuwa ni mlokole. Mnafikiri utabiri huu ni wa ulokole? Angalieni nyuma kwenye yale mafuriko ya '37, enyi watu, mliponicheka papa hapa kanisani. Nami nikasema, "Yatapanda futi ishirini na mbili juu ya Barabara ya Spring," miezi sita kabla hayajatokea. Niambieni wakati mmoja ambapo lolote liliwahi kusemwa, la BWANA ASEMA HIVI, ambalo halikuwa ni Kweli kabisa. Niambieni jambo moja ambalo amewahi kusema. Hamna kabisa! Ni Kweli, na ingali inabaki kuwa Kweli, na daima itakuwa ni Kweli.

174 Sasa hatuwezi kuwaleta . . . Nakisia kuna watu mia moja au zaidi hapa wa kuombewa. Hatuwezi kuwaleta wote mara moja. Tutawaleta tuwezao, kwa wakati mmoja, na kisha tuendelee kuwaleta hadi tutakapowaleta wote hapa. Sasa nitaanzia kwenye . . . ninaamini . . . Billy Paul hakuwepo hapa? Amerudi mle? Mwambieni atoke aje hapa. Nataka kuona kile, iwapo alisambaza . . . Ulisambaza kadi zipi za maombi? [Ndugu Billy Paul anasema, "Q, moja hadi mia moja."—Mh.] Q, Q, Q. Kadi ya maombi Q. Angalia kwenye kadi yako ya maombi. Ina Q. Moja hadi mia moja. Vema. Hatuwezi kuwaleta wote kwa wakati mmoja, lakini tunaweza kuwaleta wachache tu kwa wakati mmoja, mpaka tutakapoweza kuwaleta wote hapa. Tunawataka waje, mmoja baada ya mwingine, mpaka wote waombewe.

175 Sasa tazama. Nataka kila mtu, ndani na nje, awazie hili. Na kufungwa kwa mkutano huu, ninalikabidhi kanisa hili kwa mchungaji, Ndugu Neville, ninawakabidhi kwake, naye kwa Mungu. Ndugu Neville hapa. Nitawaalika nyote tena. Ndugu Neville ni askari hodari. Yeye ni mtumishi halisi wa Kristo. Mhubiri wa zamani wa Methodisti, naamini, mwanafunzi

kutoka Asbury, naye amefunzwa katika wanatheolojia wote, seminari ya theolojia, pamoja na ujuzi wa yale wanayofundisha. Lakini, siku moja, alifikia mahali ambapo alijua hana budi kuwa na kitu tofauti, ndipo akavuka mpaka. Yeye ndiye mchungaji hapa, mtu aliyejazwa na Roho, mhubiri kwelikweli, mwanatheolojia kwelikweli. Nami ninawaomba, watu wa mji huu, na katika jamii hii, endapo hamna kanisa, nanyi mnataka kusikia Injili halisi, njoni mumsikilize Ndugu Neville. Yeye anashindania Jambo lile lile ninaloshindania. Kweli kabisa, askari hodari kweli. Sisi sote, hapa, tunampenda Ndugu Neville. Amekuwa hapa pamoja nasi kwa muda mrefu, nasi tunampenda.

176 Sasa kama Yesu Kristo, kwa Roho, atarudi hapa usiku wa leo na kufanya mambo yale yale aliyofanya alipokuwa hapa duniani, kwa Myahudi na Msamaria, atafanya jambo lile lile kwenu ninyi Mataifa, ni wangapi wenu watasema, "Nitamwamini kwa moyo wangu wote na kulikubali papa hapa"? Sijali unashiriki kanisa gani. Hilo halina . . .

177 Unasema, "Je, unataka niache kwenda kwenye kanisa la Methodisti?" Hapana, bwana. "Baptisti?" Hapana, bwana.

178 Nenda popote unapotaka, kwa kuwa Mungu anao watoto katika kila moja la makanisa hayo. Hakika, Yeye anao. Nawe, labda, u mmoja wao. Nami ninakupenda tu sawasawa na vile ungalikuwa mshiriki wa Maskani ya Branham. Haileti tofauti hata kidogo kwangu. Mnajua hilo kwa huduma yangu, kila mahali. Ninaamini Mungu anawapenda watoto Wake, haijalishi wamebeba chapa ya aina gani. Ni kile ulicho moyoni mwako. Lakini tunawaalika tu kwenye ushirika. Mumekaribishwa kuja.

179 Sasa, mtu yeyote anajua, na ninyi watu wa Jeffersonville mnajua, baada ya mambo yote mengi ambayo yamesemwa na kufanywa, na kubashiriwa, kila moja ya hayo yakitimia kikamilifu tu kama . . . Ni wangapi hapa Jeffersonville wanaojua hilo kuwa ni kweli? Inueni mikono yenu, wanaojua mahali hapa sasa. Sasa, kwenu ninyi watu wa nje ya mji, mnaona ninachomaanisha? Ni watu wangapi wa nje ya mji ambao wamewahi kuwa katika mikutano yangu na kuona ya kwamba ilitukia jinsi tu Hiyo ilivyosema? Inueni mikono yenu, kwa watu wa Jeffersonville. Mnaona? Biblia ilisema, "Kwa kinywa cha mashahidi wawili au watatu kila neno lithibitike." Duniani kote limethibitika. Basi tunangoja nini? Tuna kila kitu mumu humu mikononi mwetu, kwa Bwana Yesu. "Ametupa vitu vyote bure."

180 Sasa tutaanza mstari wa maombi. Na kama Yesu Kristo atafanya hapa usiku wa leo . . .

181 Sasa, ni wangapi wenu wanaojua kuhusu picha ya Bwana Yesu, Nuru ile? Ninyi nyote mnajua habari Zake, hasa. Iko huko Washington, DC, iliyopigwa na mtu hodari sana ambaye Edgar Hoover amekuwa naye katika miaka michache iliyopita, George

J. Lacy, kwenye hati ya alama za vidole. Tuna sahihi ya—yake moja kwa moja kwenye karatasi. Kwamba, kweli . . . Alisema wakati mmoja alikuwa amefikiria kuwa ilikuwa ni saikolojia, nilikuwa nikiyasoma mawazo ya watu. Akasema, "Lakini, Bw. Branham, jicho la kimitambo la kamera hiyo halitapiga picha saikolojia." Kasema, "Hiyo Nuru iliigusa lenzi." Nasi tunayo yote yameandikwa kwenye karatasi, yanasambazwa pamoja na hiyo picha, hiyo Nuru iliigusa lenzi.

182 Ni wangapi wangali hai, wakati ilipoonekana mara ya kwanza mbele za watu hapa chini mtoni, nilipokuwa nikiwabatiza hao mamia huko chini siku hiyo? Katika jengo, inua mkono wako. Kuna mikono mitatu au minne, ambao wangali hai, tangu miaka iliyopita, hapa chini mtoni iliposhuka, nao Ujumbe wa Bwana ukaja. Ingali vile vile tu! Je, ilifanya vile tu ilivyosema kule? Kwamba, huduma ambayo ningekuwa nikihubiri, ingeanzisha uamsho kote ulimwenguni, kabla tu ya Kuja kwa Kristo mara ya pili. Angalieni kile imefanya. Mnaona? Hapo alitokea, hapo, Oral Roberts na hawa wengine wote. Mnaona? Na kote ulimwenguni ikaenda, kila taifa, kila watu, kila lugha. Mioto ya uamsho inawaka, ibada kuu za uponyaji. Mnaona?

183 Sasa, iweni tayari. Ndani, nje, popote ulipo, mpokee Kristo. Hivi mtampokea, usiku wa leo?

184 Sasa, tangu sasa na kuendelea, ninajikabidhi kwa Bwana Yesu, nipate kujitolea kwa Roho, kumtukuza Yesu Kristo pekee; sio mimi mwenyewe, bali Yesu Kristo; kusudi watu hawa, watu wangu, marafiki zangu, ndani na nje ya mji, wapate kujua ya kuwa Injili ambayo nimehubiri ndiyo . . . ni ya Kweli kabisa. Naye Kristo yuko hapa kuithibitisha kuwa ni Kweli, kwa Neno Lake na Roho Wake.

185 Itabidi tuwaite mmoja tu kwa wakati mmoja. Kwa hiyo tutakuwa na . . . Tutaanza na namba moja, Q namba moja. Ni nani aliye nayo? Kama—kama huwezi kusimama sasa, wazee watakubeba. Tunataka kupata kila mmoja wenu. Q namba moja. Ndugu Hickerson, Billy Paul . . . Au, ngojeni, Doc atamsaidia hapa. Q namba moja, waweza kuinua mkono wako, yeyote aliye nayo. Una hakika hizo zilikuwa ni Q? Ama, vema, loo, kunradhi. Vema. Panda huku moja kwa moja. Mwonyeshe jinsi, kupitia kwenye hayo marefu ya kanisa hapo. Q namba moja. Vema.

186 Namba mbili, inua mkono wako, tafadhali. Vema, mama anayeketi huku nyuma kabisa *hapa*. Vema, mama, njoo. Njoo papa *hapa*; kama nyote mtamruhusu. Hao wavulana hapo watakusaidia, mabawabu na kadhalika. Q mamba tatu, inua mkono wako. Namba tatu. Je, unaweza kuinua mkono wako, yeyote aliye na Q namba tatu. Angalieni kama mama huyu anayeenda hapa, kama anayo hiyo kadi. Ati hu—huna? [Dada mmoja anasema, "Ndugu Branham, niliomba nipewe kadi.

Lakini nikamwona rafiki yangu, aliyesimama na mvulana mgonjwa."—Mh.] Hu—huwezi kufanya hivyo. ["Ati siwezi?"] La. Huna budi kuishikilia na kusikiliza maagizo. Tutampata huyo mtoto mchanga, kwa vyovyote vile. Unaona? Unakuja tu wakati namba yako imeitwa. Huyo mtoto mchanga anaweza kuja wakati atakapoitwa. Unaona? Ni sawa.

187 Namba moja, mbili. Ni nani aliye na namba tatu? Inua mkono wako. Namba tatu. Namba nne.

188 Sasa, umefanya jambo la kupendeza sana, dada, yeyote yule, mama huyo aliyetaka kufanya hivyo. Mnaona? Lakini, unaona, kama—kama namba yao ikiitwa, watakuja tu kama . . . wasipoitwa, tutawapata, kwa vyovyote vile. Mnaona? Tunakutaka tu mahali pako, kusudi upate mahali pako, pia, unaona. Unaona? Vema.

189 Namba tatu. Namba nne. Namba tano. Q namba tano, inua ninii yako . . . Huko nyuma kabisa, msichana. Namba sita. Vema, huyo kijana mwanamume. Namba saba. Huyu mtu papa hapa. Namba nane.

190 Inatubidi kufanya hivi. Mnaona, huwezi kufanya hivyo; utakuwa na msongamano mkubwa, ungesema, "Kila mtu anayetaka kuombewa."

191 Hebu niwaonyeshe kitu fulani, ukitaka kuona ni kwa nini inatulazimu kuwafanyiza mstari. Kila mtu humu ndani anayetaka kuja huku na kuombewa, inueni mikono yenu, kila mtu, haidhuru wewe ni nani. Angalieni huko. Ni nani atakayekuja kwanza? Mnaona? Lazima kuwe na mtu.

192 Billy hushuka hapa, anazichukua kadi hizi, na kuzichanganya zote mbele zenu, naye humpa mtu yeyote kadi ya maombi anayetaka moja. Unaweza kupata tano, sita, na wakati mwingine tunaanza mahali pengine. Wala haileti tofauti yoyote ambapo tutaninii . . . Halafu basi hao walio huko kwenye kusanyiko kweli wanaponywa mbele ya hawa walio jukwaani, wakati mwingine. Ni wangapi wanaojua hilo, wageni na . . . Vema, hakika, halina uhusiano wowote nayo.

193 Namba sita, huyo amekuja? Namba saba. Namba nane. Ni nani aliye na kadi ya maombi nane? Tayari mmeipata? Namba tisa.

194 Nane, nambari nane, tunataka muipate sasa. Labda mtu aliye nje. Kama wako, mtu fulani ainue mkono wake, ama chochote kile, mtu fulani huko nje, asiyeweza kuingia. Namba nane. Ndugu Collins, kuna mtu yeyote huko nyuma, kadi ya maombi namba nane, anayejaribu kuingia? Vema, kadi ya maombi namba nane. Vema.

195 Nambari tisa. Kadi ya maombi tisa, inua mkono wako. Labda walitoka nje, wasingeweza kuingia. Wakiingia, waweke mstarini.

196 Namba kumi, inua mkono wako. Mtu aliye huko nyuma kabisa. Njoo, bwana. Nimefurahi kukuona ukiitwa ndani. Ulikuwa umesimama kule nyuma, viungo vikikakamaa. Namba kumi.

197 Namba kumi na moja. Inua mkono wako, yeyote aliye na kadi ya maombi Q namba kumi na moja. Vema, kumi na moja.

Kumi na mbili, Q namba kumi na mbili. Huko . . . Vema, kumi na mbili.

198 Kumi na tatu. Kumi na tatu. Inua tu mkono wako, tafadhali, ili niweze kuona. Kadi ya maombi kumi na tatu, Q kumi na tatu. Kumi na nne. Kumi na nne. Kumi na tano. Ulisambaza kadi ngapi, Billy, mia moja? Kumi na tatu, kumi na nne, na kumi na tano, hazipo. Kadi ya maombi kumi na tatu, kumi na nne, na kumi na tano, uko hapa? Kumi na tano, kumi na sita, kumi na saba, kumi na nane, kumi na tisa, ishirini.

199 Q kwanza, kisha tuchukue J, na halafu tuendelee tu kushuka mstarini. Nafikiri wanajaribu kuwapitisha hawa, kwanza, mnaona. Tukiisha kuwaita hao, tutaingia kwa wengine kadiri tunavyokuja tu. Ati nini? [Ndugu mmoja anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Ndivyo ilivyo. Mnaona, tulizisambaza kadi, asubuhi ya leo, nao hao watu hawakurudi tena, labda. Mnaona? Vema.

200 Hebu tuanze na hao wachache. Vipi . . . Uko karibu kuwa sawa na mstari wako hapo sasa? Vema. Sasa, ni nani aliye na kumi na tano, kumi na sita, kumi na saba, kumi na nane, kumi na tisa, na ishirini, katika Q? Ishirini na moja, ishirini na mbili, ishirini na tatu, ishirini na nne, ishirini na tano. Sasa iweni tu tayari, mara tu huu utakapomalizika. Tuna mstari mzima hapa sasa. Na kisha tutakuja moja kwa moja kwao, tushuke moja kwa moja mstarini, kisha turuke moja kwa moja kwenye hizo kadi zingine, za J, pale tulipoachia, na kuendelea moja kwa moja hadi tufikie mwisho wao.

201 Sasa iweni tu na kicho kabisa kwa dakika chache. Sasa, laiti tungalikuwa na nafasi ya kuketi. Laiti kungalikuwa na njia ningaliweza kufanya hivyo, lakini hatuna. Lakini, sasa, ninawatakeni muwe na uchaji vile vile. Sasa, ni mapema bado. Ni saa tatu kasoro dakika kumi. Ibada itakwisha, nusu saa nyingine. Kwa hiyo, huku ni kumalizia kwa ibada, na kwa hiyo sasa iweni na kicho kabisa. Tulieni kabisa. Msisogeesogee.

202 Basi ni wangapi humu ndani wasio na kadi ya maombi, na hata hivyo unataka kuombewa? Inueni mikono yenu. Vema, wako kila mahali. Sasa, kama huna kadi ya maombi, ninataka kukupa Maandiko fulani.

203 Wakati mmoja Bwana wetu alikuwa anaenda kumfufua msichana mdogo, aliyekufa, ambaye hakuwa amekufa bado, binti ya Zakayo. Ndipo mwanamke mmoja akasema moyoni mwake, "Ninaamini Yeye ni Mtu mtakatifu. Ninaamini Yeye ni

Masihi." Naye alikuwa ametokwa na damu kwa miaka mingi. Ndiposa akajipenyeza katikati ya umati na kuligusa vazi Lake. Umewahi kuisoma hiyo hadithi?

Ndipo Yesu akasimama, akasema, "Ni nani aliyenigusa?"

204 Naye Petro akamkemea. Akasema, "Vema, hao wote wanakugusa Wewe. Basi kwa nini unasema, 'Ni nani aliyenigusa?'"

205 Akasema, "Nimekuwa dhaifu. Uweza, nguvu, zimenitoka." Unaona linayokufanyia, ono? "Nimekuwa dhaifu. Nguvu zimenitoka."

206 Ndipo akaangalia pande zote, juu ya hilo kusanyiko, mpaka akampata huyo mwanamke. Aliogopa. Alifikiri alifanya kosa. Lakini akamtazama, akamwambia habari za kutokwa damu kwake, na kusema, "Imani yako imekuokoa." Ni wangapi wanajua kwamba hiyo ni Kweli?

207 Sasa, kwenu ninyi wasomi wa Biblia, je, Biblia inasema, ya kwamba, "Yesu Kristo sasa hivi ni Kuhani Mkuu, Kuhani wetu Mkuu, anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu"? Ni wangapi wanaojua hilo? Vema, ikiwa Yeye ni Kuhani Mkuu sasa anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu, angetendaje, ikiwa Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele? Ingemlazimu kutenda vivyo hivyo alivyotenda wakati huo. Je, hiyo ni kweli?

208 Vema, sasa, Yeye hana mwili wa nyama sasa, kwa kuwa uko kwenye mkono wa kuume wa Mungu. Bali ana miili yetu anayoitumia, na ni Roho Wake akifanya kazi kupitia sisi, kama alivyosema. "Nitakuwa pamoja nanyi, ndani yenu; kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya. Nyingi kuliko hizi mtazifanya, nyingi zaidi, kwa kuwa Mimi naenda kwa Baba." Angesimama mahali petu. Mnaona? Lakini angetutia mafuta kwa Roho.

209 Sasa, ninyi huko nje kwenye wasikilizaji, angalieni tu huku. Wala msiniangalie tu kama Ndugu Branham. Semeni tu, "Bwana Yesu, Wewe ni Kuhani Mkuu, na Wewe umo humu jengoni. Nami nataka kukugusa kwa mambo ya udhaifu wangu, nikikwambia, mimi ni mgonjwa. Nawe lithibitishe kwangu, na umruhusu tu Ndugu Branham kugeuka hivyo, kwa Roho Wako, na kuniambia kama vile ulivyomwambia mwanamke huyo. Hilo litatosha." Ninaipa imani yako changamoto, katika Jina la Bwana, kufanya hivyo. Sasa angalieni kama ni kweli ama si kweli. Mwombe Mungu hilo, uone kama linatokea hivyo tu. Sasa iweni na kicho kabisa.

210 Sasa mnaweza kuwaleta wagonjwa wenu. Au huyu ndiye yule mtu? Vema. Jambo la kwanza mstarini, sehemu hii ya mstari . . .

211 Kuna watu wengi sana humu ndani. Tunajaribu kuwaweka watu mbali, watu wa Jeffersonville; acheni tu watu wa kutoka

nje ya mji, ambao wanasongamana wapate kuingia. Kwa sababu, katika mstari wa aina hii, kama watu walikuwa wametoka hapa, karibu na Jeffersonville, wangesema, "Mbona, Ndugu Branham anawajua hao watu. Hakika, hivyo ndivyo ilivyo." Lakini, bila shaka, hawajawahi kuwa Afrika, na India, na Asia, na Ulaya, na kote ulimwenguni, katika sehemu zingine. Lakini sijui hilo.

212 Ninaamini, watu hawa wote katika mstari huu hapa sasa, wanaonekana kwangu kama hatufahamiani. Je, ninyi nyote ni wageni kwangu? Inueni tu mikono yenu kama hatufahamiani. Sawa. Hilo ni zuri. Ni wangapi kwenye kusanyiko ambao hatufahamiani, au unajua sijui shida uliyo nayo? Mtu yeyote tu, haijalishi ni nani. Hakika, hunifahamu, mnaona. Lakini Yeye anakufahamu. Sasa, sisemi ya kwamba Yeye atafanya. Lakini kama atafanya, basi hilo humfanya Yeye kuwa papa hapa.

213 Sasa, mtu huyu hapa, naamini, aliinua mkono wake, ya kwamba mimi na yeye hatufahamiani. Hatufahamiani. Sijawahi kumwona mtu huyu maishani mwangu. Nime. . . [Ndugu huyo anasema, "Sijawahi kukuona."—Mh.] Hajawahi kuniona maishani mwake hadi sasa hivi. Tumekuja humu jengoni, na tumeonana sasa kwa mara yetu ya kwanza.

214 Sasa, hii hapa picha kamili ya Filipo akienda, akimleta Nathanaeli, naye Nathanaeli akija mbele za Yesu. Sasa, si kwamba yeye ni Nathanaeli, au mimi Yesu. Sasa, msiwazie hilo. Lakini ni miaka kadhaa baadaye, kwa ahadi iliyotolewa wakati huo. Basi hawa hapa wanaume wawili ambao hawajawahi kukutana maishani, kama tu hao wanaume wawili walivyokuwa wakati huo. Basi kama Yesu anabaki yule yule, anaweza kutoa roho yake kwa imani, nami naweza kumtolea Kristo roho yangu, kwa imani, kwa kipawa cha Kiungu cha Roho Mtakatifu, ndipo anaweza kufanya mwujiza ule ule. Je, hiyo ni kweli? Na ni ya kimbinguni. Unasema, "Na mwujiza je?" Vema, ningewezaje kujua hilo, kama sijawahi kumwona? Hii hapa mikono yangu. Hatujawahi kukutana hapo awali. Sisi, hapa tumesimama, kwa mara ya kwanza. Mungu anamjua; simjui.

215 Sasa, kumbukeni, iweni mkiniombea. Sasa, wakati mwingine katika—katika nyakati hizi, Roho hutia mafuta, amekuwa akifanya hivyo sana sasa, mpaka kwa namna fulani ni. . . Vema, na—nawatakeni tu mtulie. Iweni na kicho kabisa. Angalieni. Iweni katika maombi.

216 Sasa, nakutaka tu wewe, bwana, bila kukufahamu, lakini uko hapa kwa sababu nisiyoijua. Lakini chochote kile, basi Bwana Yesu ataniambia unachotaka Kwake, bila wewe kuniambia, hilo lingemfanya Yeye tu kile nilichosema alikuwa, yeye yule jana, leo, na hata milele. Unaamini hilo? [Ndugu huyo anasema, "Hakika."—Mh.] Vema. Anaamini hilo. Na sasa kusanyiko linaamini hilo. Naye Bwana amesema angelifanya, katika Biblia Yake.

217 Sasa, hapa ndipo ninapopatikana ama nikisema Kweli pamoja na Biblia ya Mungu, au Biblia imeahidi kitu ambacho haiwezi kukitetea, ama mimi ni mnafiki; mojawapo. Mnaona? Hiyo ni kweli. Unaona mahali unapojiweka. Nimefanya hivyo mbele ya maelfu mengi, mengi sana ya watu, wakosoaji na wote. Lakini ninajua kwamba Yeye huahidi, na Yeye hutimiza ahadi Yake.

218 Ninaona Hiyo ikianza papa hapa sasa. Ninaona watu wamekuzunguka. Majukwaani katika mikutano ya nje, kamwe hatuwi na mtu karibu. Unaona? Kuna watu wagonjwa hapa. Mara tu Hiyo inapoanza, unaweza kuihisi. Ni Roho Mtakatifu. Iweni na kicho kabisa sasa, kicho tu sasa, kama tunavyoweza kunena. Naam, bwana. Bwana Yesu anatupenda sisi sote wawili, kwa maana sisi ni wanaume wawili ambao aliwafia. Na mara yetu ya kwanza kukutana. Kama una haja, Mungu anaweza kukutimizia haja hiyo, maana Yeye aliahidi atafanya hivyo.

219 Lakini sasa, huyu mtu, ikiwa ni mwaminifu moyoni mwake, anajua kwamba kuna jambo fulani linaendelea. Hawezi kuwazia ni nini hasa. Lakini Malaika yule mnayemwona kwenye ile picha, anazidi kumkaribia mtu huyo, naye anafifia kutoka kwangu. Naye huyu mwanamume anaugua ugonjwa wa moyo, pia ana kisukari. Hiyo ni kweli. Hiyo ni ROHO ASEMA HIVI. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako.

220 Sasa, kama sijawahi kukuona, ningejuaje chochote kukuhusu? Kwa namna fulani, kama vile Yeye alivyojua huko. Hiyo ni kweli? [Ndugu huyo anasema, "Hiyo ni kweli."—Mh.] Je, kusanyiko linaamini hivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."]

221 Sasa, kwa nini—kwa nini tusichukue wakati wetu, kidogo tu, ili uone kwamba haikuwa ni kitu cha kubahatisha. Hebu na tuchukue jambo lingine, na tuone tu kama Roho Mtakatifu angetufunulia jambo lingine. Hebu tuzungumze tu na yule mtu anayesimama pale, kwa dakika moja. Labda kuna kitu kingine maishani mwake, labda kitu kingine kibaya na yeye. Sijui.

222 Kwa kweli sijui nilichosema. Ingenibidi kukiona kwenye kinasa sauti hapa, maana, mnaona, ni ono, mnaona mahali alipokuwa. Naam, naliona sasa. Ni kitu fulani kuhusu damu yake. Ni sukari, naam, kisukari. Ana kisukari, na kimeenea kikawa ugonjwa wa moyo, ambao umesababisha moyo wenye fadhaa. Amekuwa nao kwa muda. Naye hatoki kwenye mji huu. Lakini anatoka Indiana, kutoka mahali karibu na mahali panapoitwa kitu kama Borden. Wewe...Ninaona Borden. Unatoka Borden. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Jambo ndilo hilo.

Na kuna shida fulani katika maisha yako.

223 Hili hapa jambo lingine. Ninaona mwanamke akitokea hapa katika ono, kwa sababu unavuti-...Ni mke wako, naye

anahitaji uponyaji. Naye anasumbuliwa na aina fulani ya kikohozi. Ni pumu, anayo.

224 Nawe una jambo baya maishani mwako, ambalo umekuwa ukijaribu kufanya. Kwa imani, wewe ni Mpentekoste, maana, wewe, ninakuona kwenye mkutano wa Kipentekoste ambapo wanapaza sauti na kupiga makofi. Na unajaribu kuachana na . . . Wewe huvuta sigara. Hilo ndilo unalojaribu kuachana nalo, kuvuta sigara. Hiyo ni kweli kabisa. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Huo ndio ukweli. Sivyo? Hakika, ndivyo. Mnaona? Je, unaamini Yeye yuko hapa sasa, yupo? Je, uko tayari kuukubali uponyaji wako?

Na tuinamishe vichwa vyetu.

225 Bwana Mungu, Wewe uliyemfufua Yesu Kristo Yule aliyeko sasa, mtu huyu, Bwana, ambaye yuko hapa ili baraka za Mungu zikae juu yake, tunaomba ya kwamba Wewe utampa shauku ya moyo wake, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

226 Rudi nyumbani kwako, uipate jinsi ulivyoamini. Hivyo ndivyo itakavyokuwa. Mungu akubariki.

227 Je, mnaamini? Mungu Mwenyezi, Yeye aliyeiandika Biblia hii, ambaye Roho Wake yupo, anajua ya kwamba sijawahi kumwona mtu huyo maishani mwangu, nijuavyo mimi, kufikia dakika hii. Lakini, najua jambo moja, Roho Mtakatifu yuko papa hapa. Sijui atakayofanya, lakini ninajua ya kwamba yuko hapa.

228 Je, huyu ndiye huyo mama? Vema. Je, tunafahamiana? Naam, wewe—wewe—wewe uliniona mikutanoni, lakini sikujui. Hiyo ni kweli. Vema. Basi, uko hapa kwa madhumuni fulani.

229 Sasa, huyu mwanamke anaweza kuwa hapa . . . Huenda akawa ni Mkristo; huenda asiwe. Huenda akawa ni mkosoaji. Kama ndivyo alivyo, angalieni tu kitakachotokea. Mnaona? Wala sijui kilichomleta hapa.

230 Mama yangu ameketi mahali fulani jengoni, mwanamke mkongwe. Je, unafikiri ningejaribu kumdhuru maskini mtu huyo? Unafikiri ningemjia kama mdanganyifu? Hakika nisingefanya hivyo. Afadhali niondoke jukwaani niende nyumbani; nimekwisha hubiri Ujumbe. Lakini hayo si yote yanayoendana na Ujumbe. Kristo ni yeye yule jana, leo na hata milele. Sijali ulimwengu unasema nini juu yake. Hatuna budi kulishindania, kwa vyovyote vile. Mungu alisema tufanye hivyo.

231 Sikujui wewe; na, bila shaka, umeketi mkutanoni, pengine palipo na mamia na mamia ya watu, nisingekuwa na njia ya kukujua. Lakini hii hapa picha sasa ya Yohana Mtakatifu 4, mwanamume na mwanamke, wakikutana kwa mara ya kwanza. Bwana wetu na yule mwanamke wa Samaria wakikutana tena. Sasa walizungumza. Aliwasiliana na roho yake, akajua shida

yake, na kumwambia, naye akamtambua kuwa ndiye Masihi. Je, ungefanya vivyo hivyo? Ungefanya.

232 Je, kusanyiko litafanya jambo lile lile, kila mwanamke huko nje? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mungu na alijalie. Naam.

233 Huyu mwanamke anaugua u—ugonjwa wa wasiwasi. Amekuwa nao kwa muda mrefu, miaka mingi iliyopita. Ningali ninaweza kumwona kama msichana. Lakini hilo silo jambo kuu analotaka niombee. Ni yabisi kavu ambayo imemlemaza. Huo ndio unaotaka niombee.

Sasa je, mnaamini?

234 Hebu tuzungumze naye kidogo zaidi. Roho Mtakatifu na alijalie hili. Huyu mwanamke kweli ni wa ja—jamii ya kigeni. Jina lake ni Hanson. Hiyo ni kweli. Mnorwe au Mswidi, mojawapo. Hutoki katika jiji hili. Unatoka mahali panapoitwa Canton. Na hapo ni katika nchi kubwa ambapo kuna ngano nyingi. Na ni Minnesota. Huko ndiko unakotoka. Hiyo ni kweli. Sasa rudi nyumbani; umeponywa. Yesu Kristo anakuponya. Waambie watu ni mambo gani mema ambayo Bwana amekutendea.

235 Nadhani hatufahamiani. [Dada huyo anasema, "Ndiyo. Nimekuwa mikutanoni, lakini wewe hunifahamu."—Mh.] Sikujui. Hapana, mama. Lakini Bwana anakujua. Uko hapa kwa kusudi fulani. Sijui. Lakini kama Bwana Yesu atanifunulia kile kilichokuleta hapa, utajua kama hiyo ni kweli. Nikija hapa na kusema, "Wewe ni mgonjwa, mwanamke." Hakika, umesimama kwenye mstari wa maombi, hiyo inaonyesha . . . [Sehemu tupu kwenye kanda.]

236 Uchunguzi wako unaonyesha kuwa una ugonjwa wa ini. Alisema ni ugonjwa wa kuumbuka ini. Hiyo ni kweli. Tuzungumze naye tu kwa dakika moja. Ninii tu . . . Je, unaamini ya kwamba Bwana Yesu, aliyezungumza na yule mwanamke kisimani, ni Yesu yule yule leo? [Dada huyo anasema, "Ndiyo."—Mh.] Unaamini? Unayo, unaonekana kuwa na roho nzuri. Wewe si wa hapa. Unatoka mashariki, kutoka Ohio. Hiyo ni kweli. Dayton, Ohio, kuja hapa. Hiyo ni kweli.

237 Naona ninii . . . Unamuombea mtu mwingine. Huyo ni mvulana. Ana ugonjwa wa moyo. Ana vidonda, pia, mvulana mwenye fadhaa. Hiyo ni kweli. Nawe unaiombea nafsi yake, kwa sababu hajaokoka. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Hiyo ni kweli. Sivyo? Umeponywa. Rudi huko. Mwambie, awe hodari sana. Yesu Kristo . . .

238 Sikujui, mama, sikufahamu. Mungu anakujua. Kama Mungu ataniambia shida yako ni nini, unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Nikimthibitisha tu Yeye. Unaona, ninachotaka kufanya ni kuwafanya watu hawa, wanaokuja kwenye mstari wa maombi, kuona ya kwamba Yeye yuko hapa.

239 Kitu fulani kilifanyika mkutanoni. Kuna wanawake wawili wamesimama pale na, wote wawili, wamevaa miwani. Mtu fulani alimgusa, kwa mambo ya udhaifu wao. Laiti ningaliweza tu kumuona huyo mwanamke, ni nini . . . Ugonjwa wako wa sikio, imekwisha sasa. Mwangalie yule mama, jinsi anavyofanana na huyu. Walikuwa wamesimama pale. Ningeweza kuwaona. Lakini mmoja alikuwa akifanya *hivi;* wala hapakuwa na kitu kwa *huyu*.

240 Sababu yake ni kwamba, mwanamke huyu anasimama kwa ajili ya mtu mwingine. Hiyo ni kweli. Naye mwanamke huyo ni jirani yako. Naye ana yabisi kavu. Nawe unasimama kwa niaba yake. Nami ninakuona ukimuombea, kwa maana hajaokoka. Na unamuombea. Huo ni ushujaa. Weka leso hiyo juu yake, uliyo nayo mkononi mwako. Mwambie asitilie shaka, na ayasalimishe maisha yake kwa Kristo, nayo yabisi kavu yake itamwacha.

241 [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . unalia nini, dada? Unamwamini Mungu? Unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Unaamini Mungu anaweza kuniambia kile unacholilia, na shauku yako ilicho? Kama unaamini hilo, inua mkono wako. Unaamini kuwa henia hiyo itamwacha? Ikiwa utaamini, itaondoka. Kuwa tu na imani. Kamwe usiwe na shaka.

242 U hali gani? Nadhani hatufahamiani. Bwana Yesu anatujua sote wawili. Wewe ni msichana hodari. Lakini huko hapa kwa ajili yako mwenyewe. Ninaona hospitali ikijitokeza, kitanda. Na ni mama yako unayemwombea, naye ametiwa uvuli wa mauti. Ana tatizo la kibofu nyongo, vivimbe. Naye ana kansa, pia, kivuli cheusi cha kansa. Chukua hiyo leso, ambayo unalilia, iweke juu yake. Na uliitie Jina la Bwana, wala usitie shaka. Kama hutatilia shaka, Mungu atamtoa huko na kumponya. Usiwe na shaka sasa. Nenda katika Jina la Bwana, na uamini.

243 Je, mumeshawishika kwamba Kristo yu hai?

244 Kuna kitu moja kwa moja . . . Loo, ni yule mwanamke anayeketi moja kwa moja nyuma huko, kwenye kiti hicho. Huumwa na kichwa. Naye amekuwa akimwomba Bwana, hapo, akijaribu kumshughulikia mtoto yule. Alikusikia, dada. Yote yamekwisha sasa. Simama tu kwa miguu yako, kumpa Mungu sifa kwa ajili yake, mama. Msifu tu Mungu kwa ajili yake. Unaona?

245 Aligusa nini? Hakunigusa mimi. Lakini alimgusa yule Kuhani Mkuu. Simjui huyo mwanamke. Sijawahi kumwona, maishani mwangu. Lakini Mungu alimponya papo hapo. Je, hiyo inamfanya Yesu yeye yule jana, leo, na hata milele? Hakika, inamfanya. Kama unaweza kuamini! Mambo yote yanawezekana kwa hao waaminio.

246 Inagusa kusanyiko, mtu fulani anaomba. Mnaona, inategemea ni wapi ambapo nguvu zimetawala, alipo Roho. Naweza tu kufuata na kusema vile Yeye asemavyo; sijui. Loo, ni yule mwanamke anayevaa miwani yake, kutokana na kulia.

Sababu ya yeye kulia, kwa kuwa Roho yuko juu yake. Huyo hapo. Hiyo shida ya matumbo ambayo umekuwa ukiteseka nayo; kuwa na imani, itakuacha wala haitarudi tena. Simjui huyo mwanamke. Sijawahi kumwona. Hakunigusa mimi. Alimgusa Kuhani Mkuu.

Kama unaweza kuamini!

247 Ilimgusa mwanamke mwingine. Nataka mtu yeyote anayetaka, angalia hapa. Mwangalieni huyu mwanamke anayelia; mwangalieni mwanamke huyo mwingine ameketi kawaida; mwangalieni huyo mwanamke mwingine kando yake, akilia. Alikuwa na ugonjwa wa moyo, maskini huyo mama anayeketi hapo hapo, ukinitazama na ninii yako . . . Naam. Hiyo ni kweli. Ulikuwa na ugonjwa wa moyo. Sivyo? Umekuacha. Imani yako ilishika moto wa Mungu, nawe ukamgusa.

Loo, ajabu hii!

248 Mnamwona mama huyo aliyeketi hapo hapo ameinamisha kichwa chake, akiomba? Mwanamke mwenye mvi, hatufahamiani, aliyeketi hapo. Naam. Uligeuka, ukamtazama. Ana ugonjwa wa kibofu nyongo. Amekuwa akimwomba Mungu amwondolee. Nawe ulikuwa unaomba basi, "Bwana, jalia aniite." Hiyo ni kweli. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Je, nilijuaje maombi yako? Umekuacha. Imani yako imekuponya. Nenda nyumbani ukapone.

249 Unaamini? Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana. Lakini huna budi kuamini.

250 Ingali inajongea sehemu hizo, kwa hao wanaoketi *hapo* ndani. Papa *hapa,* wa pili kutoka mwisho, shinikizo kuu la damu. Kama utaamini kwa moyo wako wote, dada, imekwisha. Je, unamwamini Mungu, unaliamini Neno Lake? Vema. Inua mkono wako juu. Hicho ndicho ulichokuwa ukiombea, "Bwana, jalia aniite tena, kwa shinikizo hili kuu la damu." Hatufahamiani. Ikiwa hiyo ni kweli, punga mkono wako. Vema. Limekuacha. Nenda nyumbani ukapone.

251 Unaona ni nini? Ni imani. Ikiwa unaweza kuamini! Mnaamini? Mnawaona, hao watu huko nje, hawana kadi za maombi wala chochote kile. Je, uko tayari kuamini? Je, hivyo ndivyo Bwana Yesu alivyofanya alipokuwa duniani?

252 Hapa, huyu—huyu ndiye, mtu anayekuja? Vema. Hamjui hilo linavyofanya, kwenu nyote. Kwa Maskani ya Branham, sasa angalieni tu hapa juu ya huu mkono. Mnaona? Mnajua siwi namna hiyo. Ni kitu gani? Roho wa Bwana. Ni upako.

253 Watu wengi hawaelewi maana ya upako. Wanafikiri inamaanisha kupaza sauti. Hiyo ni furaha. Nguvu zinakuja kwa uchaji. Mnaona? Hiyo ni furaha ya Bwana. Hizi ni Nguvu za Bwana; uponyaji, kuwapa afya. Angalieni kile Yeye alichomfanyia yule msichana mdogo aliyeketi hivi majuzi usiku,

akiwa amelemaa; kwa yule kipofu; kwa hao wengine, kila mahali.

254 U hali gani bwana? Nadhani hatufahamiani. Hatujuani. Sikujui, nawe hunijui. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Sawa, mara yetu ya kwanza kukutana. Iweni na kicho sasa. Huyu hapa mtu, nami pamoja naye . . . mwenye umri mdogo sana kuliko mimi, tumeinua mikono yetu, sisi kwa sisi, mbele za Mungu, ya kwamba hii ni mara yetu ya kwanza kukutana. Yesu anamjua mtu huyu. Na hapana shaka kuna shida; amesimama hapo. Sijui.

255 Lakini ikiwa nimesema kweli, ambayo Mungu ameithibitisha kwa mashahidi wengi, kwamba nimewaambia kweli, kwamba, "kwa kupigwa Kwake mliponywa." Ni wakati uliopita. Huna budi kupata imani hiyo shupavu, kupanda juu ya mambo haya.

256 Angalieni kansa ikitoweka hapa usiku wa leo! Sasa hebu angalieni tu shuhuda zikiingia kutokana nazo, hivyo vivuli vyeusi vya mauti. Daktari wako mzuri anaweza kujaribu, yote awezayo kufanya, kuyaokoa maisha yako. Lakini Mungu anaposema jambo lolote, ndivyo hivyo. Wala haikuwa ni mimi. Sina uhusiano wowote nalo.

257 Sasa kuna kama mia mbili hapa wa kuombewa. Ninataka kupumzika kwa dakika moja tu sasa. Halafu tutaanza tu kuwaombea watu, kuwaleta huku juu; si kuwapitisha upesi mstarini, bali nisimame hapa nikiwaombea. Ninataka kumwombea kila mtu anayetaka kuombewa.

258 Lakini kupitia kwenye kusanyiko, na wale walio jukwaani, ninawatakeni mtambue ya kwamba Yesu Kristo yuko hapa. Je, nyote mnafahamu hilo? Kila mtu anafahamu hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

259 Sasa, ili lipate kutatuliwa milele niani mwenu. Mimi pamoja na mtu huyu, hapa tukimwinulia Mungu mikono yetu, mara yetu ya kwanza kukutana. Ikiwa atanena siri ya moyo wake, kama tu alivyomfanyia yule mwanamke kisimani, ama kwa Filipo, ama kote kupitia huduma Yake, kama Yeye atafanya hivyo, itawathibitishia ninyi nyote, ya kwamba ni Yeye kabisa, Bwana Yesu?

260 Je, litakuthibitishia wewe, bwana? [Ndugu huyo anasema, "Naam, bwana."—Mh.] Sina njia yoyote, sijui tatizo lako. Sijui kama wewe ni mwenye dhambi au Mkristo. Nisingeweza kukwambia. Yeye hufanya hivyo; Mungu hufanya hivyo. Lakini siwezi kukwambia. Lakini kama ataniambia . . . Lakini wewe ni Mkristo. ["Naam."] Kwa maana, mara roho yako inaposhika upako wa Roho huyu aliye juu yangu, inamkaribisha, kwa hiyo najua wewe ni Mkristo.

261 Na uko chini ya kivuli kizito. Ni kasoro fulani kwenye damu. Na umekuwa kwa madaktari. Na wanataka kukufanyia

upasuaji, nao upasuaji huo ni, ninawasikia, na madaktari wawili wakishauriana, na wanataka kutoa kiungo mwilini mwako, kinachoitwa wengu. Hiyo ni kweli.

262 Nawe hutoki katika mji huu, lakini unatoka katika jiji kubwa ambako kuna taasisi kubwa ya aina fulani ya dini. Ni Wheaton. Na jina lako ni Karl Rhodes, Rhodes, kitu kama Karl Rhodes. Vema, bwana. Ikiwa utaamini kwa moyo wako wote, unaweza kurudi nyumbani kwako, naye Mungu atayaokoa maisha yako. Je, unaamini hivyo? [Ndugu huyo anasema, "Ninaamini."—Mh.]

Na tuombe.

263 Bwana Yesu, sasa ninatupilia mbali uovu huu kutoka kwa ndugu yetu. Na katika Jina la Yesu Kristo, na aishi kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Amina.

Mungu akubariki, ndugu. Nenda zako, ukishangilia!

264 Ni wangapi wanaoamini sasa kwa moyo wenu wote?

Sasa, je, hao tu ndio wote watakaoombewa? Vema.

265 Vema, shida yako ya mgongo ilikuacha ulipokuwa umeketi hapo, kwa hiyo unaweza kwenda zako, na kushangilia ukitaka. Na uendelee tu, ukisema, "Asante Bwana mwema!"

266 Nenda ukale chakula chako cha jioni. Ugonjwa wako wa tumbo ulikuacha, ukiingia mstarini, kwa hiyo unaweza kwenda kufanya upendavyo, pia. Amini tu kwa moyo wako wote.

267 Yabisi kavu yako haitakusumbua, ikiwa utaamini. Endelea mbele tu moja kwa moja, ukishangilia na kumsifu Mungu, ukipenda, ndugu. Vema. Vema.

268 Je, mnaamini kwa moyo wenu wote? Ni wangapi wanaomwamini Mungu? Sasa nitajongea tu hapa kwa muda mfupi tu. . .

*Mtu Aliyeitwa Na Mungu* SWA58-1005E
(God-Called Man)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Jumapili jioni, tarehe 5 Oktoba, 1958, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2023 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.


Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:


VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org